# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM

# KIONGOZI CHA MWEZESHAJI KWA MLEZI WA KUAMINIKA

## TOLEO LA KWANZA

**JANUARI, 2024**

# YALIYOMO

DIBAJI ..... viii

SHUKRANI ..... ix

UTANGULIZI ..... x

MADA YA KWANZA ..... 1

TAFSIRI YA DHANA ..... 1

1.1 Muda wa Kuwezesha: Dk 60 ..... 1

1.2 Malengo ya mada ..... 1

1.3 Njia za uwezeshaji ..... 1

1.4 Hatua za kuwezesha ..... 1

1.5 Maelezo ya Mada ..... 2

1.5.1 Tafsiri ya dhana mbalimbali ..... 2

1.5.2 Makundi ya watoto walio katika mazingira hatarishi ..... 4

1.5.3 Sababu za watoto kuwa katika mazingira hatarishi ..... 5

MADA YA PILI ..... 8

DHANA YA MLEZI WA KUAMINIKA ..... 8

2.1 Muda wa Kuwezesha: Dk 120 ..... 8

2.2 Malengo ya Mada ..... 8

2.3 Njia za uwezeshaji mada ..... 8

2.4 Vifaa vya kuwezeshea ..... 8

2.5 Hatua za kuwezesha ..... 8

2.6 Maelezo ya Mada ..... 9

2.6.1 Sheria na Kanuni zinazosimamia huduma za malezi toka Mlezi wa kuaminika ..... 9

2.6.2 Dhana ya Mlezi wa kuaminika ..... 9

2.6.3 Umuhimu na faida za Mlezi wa kuaminika ..... 10

2.6.4 Faida za Mpango wa Mlezi wa kuaminika ........ 10
2.6.5 Vigezo/sifa za Mlezi wa kuaminika ........ 11
2.6.6 Haki za Mlezi wa kuaminika ........ 11
2.6.7 Majukumu ya Mlezi wa kuaminika ........ 12
2.6.8 Majukumu ya Afisa Ustawi wa Jamii ........ 13
2.6.9 Muda wa mtoto kupata malezi kwa Mlezi wa kuaminika ........ 14
2.6.10 Motisha kwa Mlezi wa kuaminika ........ 14
MADA YA TATU ........ 15
HAKI ZA MTOTO ........ 15
3.1 Muda wa kuwezesha: Dk 60 ........ 15
3.2 Malengo ya Mada ........ 15
3.3 Njia za uwezeshaji ........ 15
3.4 Hatua za kuwezesha ........ 15
3.5 Maelezo ya Mada ........ 15
3.5.1 Chimbuko la Haki za Mtoto ........ 15
3.5.2 Haki za mtoto zimegawanyika katika makundi makuu matano ........ 16
3.5.3 Wajibu wa Mtoto ........ 17
MADA YA NNE ........ 18
KANUNI ZA MAADILI ZA KUHUDUMIA WATOTO ........ 18
4.1 Muda wa kuwezesha: Dk 60 ........ 18
4.2 Malengo ya Mada ........ 18
4.3 Njia za uwezeshaji mada ........ 18
4.4 Vifaa vya kuwezesha ........ 18
4.5 Hatua za kuwezesha ........ 18
4.6 Maelezo ya Mada ........ 19

4.6.1 Kanuni na maadili ya kufanya kazi na watoto ..... 19

MADA YA TANO ..... 21

ULINZI NA USALAMA WA MTOTO ..... 21

5.1 Muda wa kuwezesha: Dk 120 ..... 21

5.2 Malengo ya Mada ..... 21

5.3 Njia za uwezeshaji ..... 21

5.4 Hatua za kuwezesha ..... 21

5.5 Maelezo ya Mada ..... 22

5.5.1 Dhana ya ulinzi na usalama wa mtoto ..... 22

5.5.2 Aina za unyanyasaji na ukatili dhidi ya watoto ..... 22

5.5.3 Sababu zinazochangia unyanyasaji na ukatili kwa watoto ..... 27

5.5.4 Hatua za kuchukua pale mtoto anapobainika kuwa amefanyiwa ukatili au yuko katika hatari ya kufanyiwa ukatili ..... 28

5.5.5 Mamlaka zenye dhamana ya kushughulikia ulinzi na usalama wa mtoto ..... 28

5.5.6 Wadau muhimu ambao wanawajibika katika kushughulikia masuala ya ulinzi na usalama wa mtoto ..... 29

MADA YA SITA ..... 30

MALEZI, MAKUZI NA MAENDELEO YA AWALI YA MTOTO ..... 30

6.1 Muda wa kuwezesha: Dk 120 ..... 30

6.2 Malengo ya Mada ..... 30

6.3 Njia za uwezeshaji ..... 30

6.4 Hatua za kuwezesha ..... 30

6.5 Maelezo ya Mada ..... 31

6.5.1 Maendeleo ya Mtoto ..... 31

6.5.2 Hatua za Ukuaji wa Mtoto ..... 31

6.5.3 Huduma muhimu za Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto (MMMAM) ..... 33

6.5.4 Uchangamshi wa awali unahusisha mambo yafuatayo: ... 34

6.5.5 Uchangamshi wa awali unapaswa kufanywa na Mzazi/Mlezi kwa kutenda vitendo vilivyokusudiwa na kwa kujirudia kwa kuzingatia umri wa mtoto kama ifuatavyo: ... 34

6.5.6 Wadau na taasisi ambapo huduma muhimu zinapatikana ... 35

MADA YA SABA ... 37

AFYA YA AKILI NA MSAADA WA KISAIKOLOJIA NA KIJAMII ... 37

7.1 Muda wa kuwezesha: Dk 120 ... 37

7.2 Malengo ya Mada ... 37

7.3 Njia za uwezeshaji ... 37

7.4 Hatua za kuwezesha ... 37

7.5 Maelezo ya Mada ... 38

7.5.1 Mahitaji ya kisaikolojia na kijamii ... 38

7.5.2 Michezo ya watoto inaweza kuainishwa kwa : ... 43

7.5.3 Namna ya kumsaidia Mtoto mwenye uhitaji wa Huduma ya Msaada wa Kisaikolojia na Kijamii ... 44

7.5.4 Athari kwa Mtoto aliyekosa Mahitaji ya Kisaikolojia na Kijamii ... 45

7.5.5 Athari kwa Jamii ... 45

MADA YA NANE ... 47

HUDUMA KWA MTOTO MWENYE MSONGO ... 47

8.1 Muda wa kuwezesha: Dk 60 ... 47

8.2 Malengo ya Mada ... 47

8.3 Njia za uwezeshaji ... 47

8.4 Hatua za uwezeshaji ... 47

8.5 Maelezo ya Mada ... 48

8.5.1 Kumsaidia Mtoto mwenye Msongo ... 48

8.5.2 Vyanzo vya msongo ... 48

8.5.3 Dalili za Mtu mwenye Msongo ........ 48

8.5.4 Jinsi ya kumsaidia Mtoto aliye katika mazingira hatarishi mwenye Msongo ........ 49

8.5.5 Mambo ambayo yanaweza kumwezesha mtoto aliye katika mazingira hatarishi kupunguza msongo ........ 49

MADA YA TISA ........ 50

MAREKEBISHO YA TABIA ........ 50

9.1 Muda wa kuwezesha: Dk 90 ........ 50

9.2 Malengo ya Mada ........ 50

9.3 Njia za uwezeshaji ........ 50

9.4 Hatua za Uwezeshaji ........ 50

9.5 Maelezo ya Mada ........ 51

9.5.1 Malengo ya marekebisho ya tabia ........ 51

9.5.2 Mbinu za marekebisho ya tabia ya Mtoto ........ 51

9.5.3 Mawasiliano chanya ya Mzazi /Mlezi na mtoto ........ 52

9.5.4 Mbinu za kumuadabisha mtoto ........ 52

9.5.5 Faida za Kumrekebisha Mtoto tabia ........ 53

MADA YA KUMI ........ 54

UTAMBUZI WA WADAU ........ 54

10.1 Muda wa kuwezesha: Dk 90 ........ 54

10.2 Malengo ya Mada ........ 54

10.3 Njia za uwezeshaji ........ 54

10.4 Vifaa vya kuwezeshea ........ 54

10.5 Hatua za kuwezesha ........ 54

**10.6 Maelezo ya Mada** ........ 55

10.6.1 Baadhi ya wadau wanaoweza kusaidia utoaji wa huduma kwa watoto ........ 55

10.6.2 Umuhimu wa Wadau ........ 56

10.6.3 Majukumu ya wadau ..... 56

MADA YA KUMI NA MOJA ..... 59

KUIMARISHA UCHUMI WA KAYA ..... 59

11.1 Muda wa kuwezesha: Dk 120 ..... 59

11.2 Malengo ya Mada ..... 59

11.3 Njia za uwezeshaji ..... 59

11.4 Hatua za kuwezesha ..... 59

11.5 Maelezo ya Mada ..... 60

11.5.1 Maana ya rasilimali ..... 60

11.5.2 Aina za rasilimali ..... 60

11.5.3 Namna ya kubuni na kuendesha miradi midogomidogo itakayosaidia kuongeza kipato katika Kaya ..... 60

11.5.4 Masuala ya kuzingatia wakati wa kuanzisha mradi ..... 61

11.5.5 Umuhimu wa kujiunga katika vikundi vya kiuchumi na biashara ndogo ndogo kwa lengo la kuimarisha uchumi wa Kaya /Familia ..... 61

MADA YA KUMI NA MBILI ..... 63

HUDUMA KWA WATU WENYE ULEMAVU ..... 63

12.1 Muda wa kuwezesha: Dk 120 ..... 63

12.2 Malengo ya Mada ..... 63

12.3 Njia za uwezeshaji ..... 63

12.4 Hatua za kuwezesha ..... 63

12.5 Maelezo ya Mada ..... 64

12.5.1 Mtoto mwenye ulemavu ..... 64

12.5.2 Haki za watoto wenye ulemavu ..... 64

12.5.3 Utambuzi wa awali wa mtoto mwenye ulemavu ..... 64

12.5.4 Vyanzo vya ulemavu ..... 64

12.5.5 Aina za Ulemavu........ 65

12.5.6 Namna ya kuzuia Ulemavu........ 65

12.5.7 Vifaa vya kujimudu /visaidizi........ 66

12.5.8 Tiba........ 67

12.5.9 Lishe........ 67

**12.6 Unasihi**........ 67

**DIBAJI**

Mwongozo huu umeandaliwa maalum kwa ajili ya Maafisa Ustawi wa Jamii na wadau wengine wanaotoa huduma kwa watoto walio katika mazingira hatarishi ili waweze kuwajengea uwezo walezi wa kuaminika katika ngazi ya jamii ili watoe huduma bora za malezi kwa watoto watakaowapokea kwa ajilli ya kuwalea.

Uzoefu umeonesha kuwa walezi wa kuaminika wamekuwa na changamoto kubwa katika malezi ya watoto katika maeneo mbalimbali kama vile ulinzi na usalama wa mtoto, utoaji wa msaada wa Kisaikolojia na Kijamii, Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto na marekebisho ya tabia.

Juhudi kadhaa zimekuwa zikichukuliwa na wadau mbalimbali kuhakikisha watoto walio katika mazingira hatarishi wanapata malezi, lakini kila mdau amekuwa akitekeleza shughuli zake kwa utaratibu tofauti. Kwa kuzingatia hilo Serikali imeandaa mwongozo huu ili kuimarisha uratibu na kuelekeza wadau wote ili waweze kutekeleza shughuli zao katika utaratibu na viwango vya ubora hatimaye kuimarisha huduma ya malezi kwa watoto hao.

Mwongozo huu utakuwa ni rejea itakayotumika na wadau wote katika kufundisha walezi wa kuaminika.

Dkt. Seif Abdallah Shekalaghe

Katibu Mkuu
**Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum**

## SHUKRANI

Maandalizi ya mwongozo huu wa kufundishia Walezi wa kuaminika katika ngazi ya jamii ni matokeo ya juhudi kubwa zilizofanywa na wadau mbalimbali. Hivyo Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum inapenda kutoa shukrani za kipekee kwa Rais Ofisi ya Rais – Tawala Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI), Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera Uratibu na Watu Wenye Ulemavu, Shirika la Kuhudumia Watoto Duniani (UNICEF), shirika la SOS Children Villages na Railway Children Africa (RCA) kwa msaada wa kitaalamu na kifedha ambao umewezesha kukamilisha uandaaji wa mwongozo huu.

Shukurani za dhati ziende kwa Kamishna Masidizi wa Ustawi wa Jamii na Watoto kwa kusimamia na kutoa ushauri uliofanikisha ukamilishaji wa Mwongozo huu.

Mwisho lakini sio kwa umuhimu natoa shukrani za pekee kwa timu ya wataalamu pamoja na wadau wote ambao kwa njia moja au nyingine wameshiriki kuandaa na kukamilisha mwongozo huu muhimu wa mafunzo kwa Walezi wa Kuaminika katika ngazi ya jamii



**Dkt. Nandera E. Mhando**

**Kamishna wa Ustawi wa Jamii**

## UTANGULIZI

Malezi kutoka kwa Mlezi wa kuaminika ni mpango ulioanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Mtoto namba 21 ya mwaka 2009 kama njia mbadala ya malezi kwa watoto walio katika mazingira hatarishi ambao kwa sababu mbalimbali hawawezi kuishi na Wazazi/Walezi wao. Uhitaji wa malezi na ulinzi kwa watoto walio katika mazingira hatarishi umeongezeka kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo; unyanyasaji na ukatili, kukinzana na sheria, migogoro na kuvunjika kwa ndoa, wazazi/familia kutengana na watoto na kutokuwa na mawasiliano ya karibu, umaskini wa kipato katika ngazi ya familia, wazazi/walezi kuugua kwa muda mrefu na kushindwa kutoa huduma kwa watoto.

Kutokana na changamoto hizo watoto wengi wamekosa malezi ya wazazi ambayo ni muhimu katika makuzi na maendeleo ya mtoto, kiakili, kijamii na kihisia. Hali hii imesababisha watoto wengi kulelewa katika makao ya watoto badala ya familia. Kutokana na sababu hizo Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo imeanzisha mpango wa Mlezi wa kuaminika ili watoto waweze kupata malezi ya familia. Mpango huu umeanza kutekelezwa katika baadhi ya Halmashauri nchini na kuonyesha mafanikio makubwa ikiwa ni pamoja na kupunguza idadi ya watoto wanaopelekwa kwenye makao ya watoto na watoto wanaoishi na kufanya kazi mitaani.

Pamoja na mafanikio hayo bado kuna changamoto katika utoaji wa malezi, matunzo na ulinzi kwa watoto wakiwa katika familia za walezi wa kuaminika hasa kwa kuzingatia tabia za watoto na mazingira waliyokulia.

Katika kuboresha utekelezaji wa mpango huu Wizara imeandaa mwongozo unaolenga kuwajengea uwezo walezi wa kuaminika ili waweze kutoa huduma za malezi, matunzo na ulinzi kwa watoto walio katika mazingira hatarishi.

Watumiaji wa mwongozo huu ni Maafisa Ustawi wa Jamii katika Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Wadau wa Maendeleo, Asasi za Kiraia na Mashirika ya Dini ili waweze kuwajengea uwezo walezi wa kuaminika waliotambuliwa na kuthibitishwa katika Halmashauri husika kulea watoto walio katika mazingira hatarishi.

Mwongozo huu una jumla ya mada 12 kama ifuatavyo;

i. Tafsiri ya Dhana
ii. Dhana ya Mlezi wa kuaminika
iii. Haki za Mtoto
iv. Kanuni za maadili za kuhudumia Watoto
v. Ulinzi na Usalama wa Mtoto
vi. Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto
vii. Afya ya akili na Msaada wa Kisaikolojia na kijamii
viii. Huduma kwa mtoto mwenye msongo wa mawazo
ix. Marekebisho ya tabia
x. Utambuzi wa wadau
xi. Kuimarisha uchumi wa Kaya
xii. Huduma kwa watu wenye ulemavu

Maandalizi ya mwongozo huu yamehusisha wadau mbalimbali katika hatua tofauti kutoka Serikali Kuu, Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wadau wa Maendeleo, Asasi za Kiraia, walezi na watoto.

## MADA YA KWANZA
## TAFSIRI YA DHANA

**1.1 Muda wa Kuwezesha:** Dk 60

### 1.2 Malengo ya mada

Ifikapo mwisho wa mada hii washiriki wataweza:

- Kuelewa tafsiri za dhana mbalimbali
- Kuelewa makundi ya watoto walio katika mazingira hatarishi

### 1.3 Njia za uwezeshaji

- Mhadhara mfupi
- Bungua bongo
- Majadiliano katika vikundi
- Majadiliano ya pamoja

### 1.4 Hatua za kuwezesha

**Hatua ya 1:** Toa maelezo ya utangulizi wa mada.

**Hatua ya 2:** Ongoza washiriki kubungua bongo juu ya maana ya dhana zifuatazo: Mtoto, Mlezi wa kuaminika, Malezi ya kambo, Watoto walio katika mazingira hatarishi na Watoto walio katika mkinzano na sheria.

**Hatua ya 3:** Wagawe washiriki katika vikundi wajadili mambo yafuatayo na waandike katika bango kitita:

- Makundi ya watoto walio katika mazingira hatarishi na watoe mifano.
- Sababu za watoto kuwa katika mazingira hatarishi.

**Hatua ya 4:** Wezesha washiriki kuwasilisha kazi za vikundi na kufanya majadiliano ya pamoja.

**Hatua ya 5**: Hitimisha kwa kutoa muhtasari.

## 1.5 Maelezo ya Mada

### 1.5.1 Tafsiri ya dhana mbalimbali

**Mtoto**

Kwa mujibu wa Sheria ya Mtoto namba 21 ya mwaka 2009 iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2019, mtoto ni mtu yoyote aliye chini ya umri wa miaka kumi na nane.

**Haki za Mtoto**

Ni stahili ambayo mtoto anapaswa kupewa au kutoa kutokana na ubinadamu au utoto wake bila kujali kabila, jinsi, dini, rangi ya ngozi, hali kama ulemavu au umasikini. Haki hizo ni pamoja na haki ya kuishi, kuendelezwa, kulindwa, kushiriki na kushirikishwa.

**Mlezi wa kuaminika**

Ni mtu mzima mwenye maadili, hekima na akili timamu ambaye siyo ndugu wa mtoto na ana uwezo wa kumtunza mtoto na amethibitishwa na Afisa Ustawi wa Jamii kuwa na uwezo wa kutoa malezi kwa mtoto.

**Mtoto aliye katika mkinzano na sheria**

Ni mtoto ambaye kutokana na sababu moja au nyingine amefanya makosa na kufikishwa kwenye mfumo wa sheria kama Mahakamani au Polisi.

**Maana ya msongo**

Msongo ni aina ya shinikizo la kiakili ambalo humfanya mwathirika kupata matatizo ya kimaono na kiutendaji.

Mtu mwenye msongo hupata matatizo ya kisaikolojia yanayojionyesha kwa hali mbalimbali zikiwemo:

- Kushindwa kufikiri ipasavyo na hivyo kuwa na utendaji hafifu; kwa mfano, kushindwa kujifunza masomo ipasavyo.
- Kuwa na uhusiano hasi na watu wengine kutokana na hali ya hasira, kujitenga n.k
- Kuwa na malalamiko ya mara kwa mara kuhusu afya au watu wengine.

**Uchepushaji**

Uchepushaji ni mchakato wa kumtoa mtoto aliyekinzana na sheria kutoka mfumo rasmi wa kuendesha Mashauri ya Jinai (kutoka Kituo cha Polisi, Mahakamani au Mahabusu ya Watoto) na kupelekwa kwenye Kituo cha Marekebisho ya tabia. Aidha, Uchepushaji huu utafanyika tu iwapo mtoto amekiri kosa na kuridhia kwenda kwenye mpango wa Marekebisho ya tabia.

**Malezi**

Ni matendo yote chanya yanayofanywa na mzazi/mlezi kwa mwelekeo chanya ili kumwezesha mtoto kukua katika nyanja zote (kimwili, kiakili, kihisia, kimaadili na kijamii) ili aweze kukubalika na jamii. Aidha, inahusisha mchakato wa maandalizi ya mtoto utakaomwezesha kukua, kukubalika na kushiriki katika shughuli za kijamii na kitamaduni kwa kumlinda, kumjamiisha na kumpatia mahitaji na huduma za msingi.

**Malezi ya kambo**

Ni malezi ya muda na ya hiari yanayotolewa na familia au mtu binafsi ambaye hana uhusiano na mtoto huyo na yuko tayari kutoa malezi, matunzo na ulinzi kwa mtoto baada ya kukabidhiwa na Kamishna wa Ustawi wa Jamii.

**Ulinzi na usalama wa mtoto**

Ni shughuli zote zinazolenga kuzuia ukatili na unyanyasaji wa mtoto na kutoa huduma kwa watoto waliofanyiwa vitendo au walio katika hatari ya kufanyiwa vitendo vya ukatili na unyanyasaji.

**Mtoto aliye katika mazingira hatarishi**

Ni mtoto ambaye tayari yuko hatarini au anaweza kuwa hatarini kwa kukosa haki zake za msingi. Kwa kiasi kikubwa, watoto walio katika mazingira hatarishi huwa wamekosa malezi ya kifamilia kutokana na wazazi kufariki, kutelekezwa na wazazi, kutumikishwa, kufanyiwa vitendo vya ukatili na unyanyasaji, kuwa na ulemavu au umaskini uliokithiri. Watoto hao kwa kawaida huishi katika shida, wakikosa haki zao za msingi zikiwemo Malazi, Mavazi, Chakula, Elimu na Matibabu. Mazingira mengine hatarishi humlazimisha mtoto kuingia katika vitendo vya ulevi wa pombe na madawa ya kulevya, kuamua kuishi mtaani, ajira na vitendo vingine vinavyohatarisha afya na maendeleo yake.

**Ulemavu**

Ni hali yoyote ya dosari katika viungo vya mwili au akili ambayo husababisha mtu kushindwa kutenda mambo ambayo angeweza kuyafanya hivyo humletea mtu kizuizi katika utekelezaji wa majukumu yake katika jamii.

### 1.5.2 Makundi ya watoto walio katika mazingira hatarishi

Makundi ya watoto walio katika mazingira hatarishi ambao wanaweza kupatiwa malezi kwa Mlezi wa kuaminika ni pamoja na :

i. Yatima au alietelekezwa na ndugu zake.

ii. Ametelekezwa au ametendewa visivyo na Mlezi wake au Wazazi.

iii. Ana Mzazi/Mlezi asiyetoa malezi sahihi.

iv. Analelewa na Mzazi/Mlezi ambaye kutokana na tabia za kihalifu au ulevi hawezi kumlea mtoto.

v. Mzururaji na hana makazi au sehemu ya kuishi.

vi. Ombaomba au anaishi kwa kutegemea misaada kwa kisingizio cha kuimba, kucheza, kufanya maonyesho, kuuza kitu chochote au vinginevyo.

vii. Anaambatana na mtu yeyote ambaye ni ombaomba.

viii. Analelewa na Mzazi asiye na uwezo au Mzazi fukara.

ix. Mara kwa mara anaambatana na mhalifu sugu au kahaba.

x. Anaishi kwenye nyumba au sehemu ya nyumba inayotumiwa na makahaba kwa lengo la kufanya ukahaba.

xi. Ni mtu amabaye kupitia kwake kosa limetendwa au jaribio la kosa chini ya Sheria ya Usafirishaji Haramu wa Binadamu.

xii. Amekuwa akifanya jambo au kushawishi kufanya mambo yaliyo kinyume na maadili.

xiii. Yupo chini ya umri unaomfanya awajibike kijinai na amehusika kutenda kosa kubwa la jinai.

xiv. Analelewa na mtu mwenye ulemavu ambaye ulemavu huo unamfanya asiweze kumpa mtoto malezi stahili.

xv. Watoto wanaotumikishwa.

xvi. Watoto waliokinzana na walio katika hatari ya kukinzana na sheria.

xvii. Watoto wanaojilea.

xviii. Endapo mtoto huyo yupo katika mazingira mengine yoyote kama ambavyo Kamishna wa Ustawi wa Jamii ataamua.

### 1.5.3 Sababu za watoto kuwa katika mazingira hatarishi

Zipo sababu mbalimbali za watoto kuwa katika mazingira hatarishi. Baadhi ya sababu hizo ni pamoja na:

i. **Umaskini uliokithiri hasa katika ngazi ya Familia/Kaya**

Umaskini uliokithiri katika ngazi ya familia unasababisha watoto kukosa mahitaji ya msingi kama vile chakula, mahitaji ya shule na matibabu.

ii. **Mila na desturi zinazoleta madhara**

Zipo baadhi ya mila na desturi ambazo zina athari kwa watoto na kuwasababishia kuwa katika mazingira hatarishi. Miongoni mwa mila na desturi hizo ni pamoja na:

- Mila ya kurithi wajane.
- Wasichana kuolewa katika umri mdogo (chini ya miaka kumi na nane) ili Wazazi wapate kipato.
- Mitala; kuwa na wake wengi bila kuwa na uwezo wa kutunza watoto ambao ni matokeo yake.
- Ukeketaji.
- Kutokutoa haki za msingi kwa usawa, mfano watoto wa kike kupewa kazi nyingi zaidi kuliko watoto wa kiume au watoto wa kiume kupewa fursa zaidi kuliko watoto wa kike.

iii. **Imani za kishirikina**

Imani za kishirikina husababisha watoto kufanyiwa vitendo vya unyanyasaji na ukatili, mfano kukata na kutumia viungo vya watoto wenye ualbino; watoto kuhusishwa katika vitendo vya kishirikina na ubakaji wa watoto wadogo kwa tamaa ya kupata mali.

iv. **Kudhoofika kwa mfumo wa malezi ya jadi**

Awali jamii ilizoea kutunza watoto wa ndugu pale ambapo wazazi wamekuwa wagonjwa kwa muda mrefu, ama wamefariki jambo ambalo kwa sasa limedhoofika kwa kiasi kikubwa.

v. **Migogoro na kuvunjika kwa ndoa**

Mara nyingi ndoa zinapokuwa kwenye migogoro au zinapovunjika wanaoathirika ni watoto kwa kukosa malezi, matunzo na ulinzi.

vi. **Athari zinazotokana na magonjwa mbalimbali**

Magonjwa haya ni kama vile UKIMWI na UVIKO 19 ambayo yameleta athari nyingi ambazo zimesababisha familia kutumia fedha nyingi na rasilimali nyingine za familia hivyo kubaki katika hali ngumu zaidi. Aidha vifo vilivyotokea vimewaacha watoto wengi yatima na familia kusambaratika. Watoto wengine huzaliwa na maambukizi na kukosa huduma.

vii. **Unyanyasaji na ukatili**

Baadhi ya watoto katika jamii wanatelekezwa, wanateswa na wanapewa adhabu za kikatili kama vile kuunguzwa moto, kupigwa na kukatwa baadhi ya viungo, kunyimwa chakula, kubakwa na kufanyiwa ukatili wa kijinsia, hali inayopelekea wawe kwenye mazingira hatarishi.

viii. **Kukosa stadi za malezi kwa Wazazi/Walezi**

Wazazi/Walezi kutokuwa na uelewa wa kutosha kuhusiana na Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto kunasababisha kushindwa kutoa malezi stahiki kwa watoto.

ix. **Wazazi/Walezi kutowajibika ipasavyo**

Uvivu, ulevi wa kupindukia kwa baadhi ya Wazazi/Walezi na kutojishughulisha na shughuli yoyote ya kuwaletea kipato kunasababisha watoto kukosa mahitaji ya msingi na hivyo kuingia katika mazingira hatarishi.

x. **Kutowapatia chanjo watoto walio chini ya miaka mitano na wajawazito kutopata huduma za kliniki.**

Magonjwa mengi yanaweza kuzuilika kwa chanjo ikitolewa kwa wakati unaostahili kwa watoto na wajawazito. Chanjo isipotolewa kwa usahihi na kwa wakati watoto

wanaweza kupata baadhi ya magonjwa na ulemavu kwa mfano ugonjwa wa akili na kupooza hivyo kuwafanya wawe katika mazingira hatarishi.

xi. **Matumizi yasiyo sahihi ya Mitandao ya Kijamii**

Matumizi ya mitandao yanawaweka watoto katika hatari kubwa ya ukatili na unyanyasaj. Mitandao ya Kijamii ina taarifa na picha nyingi zisizo na maadili ambazo watoto wanajikuta wahanga na wamekuwa na urahibu wa mitandao ambayo imewapa nafasi ya kujifunza na kuwa tegemezi wa mitandao.

xii. **Watoto kujiingiza kwenye michezo ya kubeti na kamari**

Badala ya watoto kwenda Shule wanajihusisha na michezo ya kubeti na kamari ambayo inawanyima fursa ya kujiendeleza kielimu. Jambo ili linawasababisha watoto kuwa katika hatari ya kukinzana na sheria.

# MADA YA PILI
# DHANA YA MLEZI WA KUAMINIKA

**2.1 Muda wa Kuwezesha:** Dk 120

## 2.2 Malengo ya Mada

Ifikapo mwisho wa mada hii washiriki wataweza kufahamu:

- Sheria na Kanuni zinazosimamia huduma za malezi toka kwa Mlezi wa kuaminika
- Umuhimu wa Mlezi wa kuaminika
- Sifa/vigezo vya Mlezi wa kuaminika
- Haki za Mlezi wa kuaminika
- Majukumu ya Mlezi wa kuaminika
- Majukumu ya Afisa Ustawi wa Jamii

## 2.3 Njia za uwezeshaji mada

- Mihadhara mifupi
- Bungua bongo
- Mawasilisho ya mada
- Majadiliano katika vikundi vidogo
- Majadiliano ya pamoja

## 2.4 Vifaa vya kuwezeshea

- Bango kitita
- Kalamu za wino mzito
- Vitini vya sheria
- Projecta

## 2.5 Hatua za kuwezesha

**Hatua ya 1:** Tambulisha mada na malengo yake.

**Hatua ya 2:** Ongoza washiriki kubungua bongo kuhusu maana ya Mlezi wa kuaminika na tofauti yake na mlezi wa kambo.

**Hatua ya 3:** Toa ufafanuzi kuhusu maana ya Mlezi wa kuaminika na tofauti yake na Mlezi wa kambo.

**Hatua ya 4:** Wapitishe washiriki na kutoa ufafanuzi kuhusu umuhimu wa Mlezi wa kuaminika, majukumu ya Mlezi wa kuaminika na majukumu ya Afisa Ustawi wa Jamii.

**Hatua ya 5:** Wagawe washiriki kwenye vikundi ili wajadiliane kuhusu yafuatayo:

- Sifa/vigezo vya Mlezi wa kuaminika.
- Haki za Mlezi wa kuaminika.

**Hatua ya 6:** Wezesha vikundi kuwasilisha majibu.

**Hatua ya 7:** Toa ufafanuzi kuhusiana na mada zilizojadiliwa.

**Hatua ya 8:** Toa maelezo ya kina kuhusu muda wa mtoto kuwa katika malezi kwa Mlezi wa kuaminika.

## 2.6 Maelezo ya Mada

### 2.6.1 Sheria na Kanuni zinazosimamia huduma za malezi toka Mlezi wa kuaminika

i. Sheria ya Mtoto Na. 21 ya mwaka 2009 iliyofanyiwa marekebisho 2019.

ii. Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971.

iii. Kanuni za Mlezi wa kuaminika za Mwaka 2019.

iv. Kanuni ya Malezi ya Kambo ya mwaka 2012.

v. Kanuni ya Uendeshaji wa Mashauri ya Watoto Mahakamani 2014.

### 2.6.2 Dhana ya Mlezi wa kuaminika

Sheria ya Mtoto Na. 21 ya mwaka 2009 kifungu cha 3 inafafanua kuwa; Mlezi wa kuaminika ni Mtu mzima, mwadilifu na mwenye msimamo na akili timamu ambaye si ndugu wa mtoto ambaye ana uwezo wa kumtunza mtoto na ambaye amethibitishwa na Afisa Ustawi wa Jamii kuwa na uwezo wa kumpatia mtoto malezi, matunzo na ulinzi anaostahili.

Kanuni za Mlezi wa kuaminika zinamtaka Afisa Ustawi wa Jamii wa kila Halmashauri kuhakikisha uwepo wa Walezi wa kuaminika ili kutoa malezi ya muda kwa watoto wenye uhitaji katika Halmashauri husika.

| |
|---|
| **Angalizo:** Zingatia maelezo katika kitabu cha rejea kwa kila mada |

**Jedwali Na. 1: Tofauti kati ya Mlezi wa kuaminika na Mlezi wa kambo**

| Mlezi wa kuaminika | Mlezi wa kambo |
|---|---|
| • Hawalipwi ujira ila wanaweza kupewa motisha kulingana na mazingira.<br>• Atatoa malezi kwa mtoto kwa kipindi kisichozidi miezi 6.<br>• Anachaguliwa na kuthibitishwa na Afisa Ustawi wa Jamii wa Halmashauri husika.<br>• Anaombwa kutoa huduma ya malezi.<br>• Ni huduma ya Malezi ya dharura. | • Halipwi ujira.<br>• Mtoto huwekwa chini ya malezi ya kambo kwa muda wa kipindi kisichopungua miezi sita kwa mwenye nia ya kuasili. Kwa anaetaka kutoa Malezi ya kambo ya kawaida atamlea mtoto hadi atakapofikia miaka 18 au 21 kama anaendelea na mfumo rasmi wa elimu (LCA 18(4).<br>• Anathibitishwa na Kamishna wa Ustawi wa Jamii.<br>• Mhusika anaomba mwenyewe kutoa huduma ya malezi, matunzo na ulinzi kwa mtoto husika.<br>• Ni huduma ya malezi ya muda. |

### 2.6.3 Umuhimu na faida za Mlezi wa kuaminika

Watoto wengi wamekosa malezi na huduma katika familia kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo kufiwa na wazazi, utelekezaji wa watoto, hali duni kwa baadhi ya familia kutokana na magonjwa ya muda mrefu kwa Wazazi/Walezi, mfarakano baina ya Wazazi/Walezi na ukatili dhidi ya Watoto. Uwepo wa mpango wa Mlezi wa kuaminika umesaidia watoto hao kupata malezi, matunzo na huduma wanazostahili.

#### 2.6.4 Faida za Mpango wa Mlezi wa kuaminika

i. Kutoa huduma za dharura za malezi, matunzo na ulinzi kwa mtoto/watoto wenye uhitaji wa huduma hiyo.

ii. Kutoa hifadhi ya muda kwa watoto wenye uhitaji na kuwapatia fursa ya kupata malezi ya kifamilia wakati wanahudhuria programu mbalimbali wakati changamoto zao zikiendelea kushughulikiwa.

iii. Kutoa makazi kwa watoto walio katika mkinzano na Sheria ili kuwaepusha kupelekwa katika mahabusu za watoto pale ambapo wamepewa dhamana.

iv. Kupunguza ongezeko la watoto wanaoishi na kufanya kazi mitaani na kwenye makao ya kulelea Watoto.

### 2.6.5 Vigezo/sifa za Mlezi wa kuaminika

i. Awe na umri usiopungua miaka 25 na usiozidi miaka 65.
ii. Awe na makazi ya kudumu.
iii. Awe na uelewa kuhusu athari wanazopata watoto kutokana na migogoro ya kifamilia.
iv. Awe ni mtu mwenye huruma na upendo kwa watoto walio katika mazingira hatarishi.
v. Awe na uwezo wa kutoa huduma za msingi kwa mtoto ikiwemo malazi, chakula na mavazi.
vi. Awe muadilifu (asiwe mlevi wala mtumiaji wa dawa za kulevya na asijihusishe biashara ya ngono).
vii. Awe na akili timamu (asiwe na matatizo ya Afya ya Akili).
viii. Athibitishwe na Afisa Mtendaji wa Kijiji/Mtaa.
ix. Awe na mdhamini anayemfahamu kwa kipindi kisichopungua miaka 3.
x. Kwa mwanaume mwenye mke zaidi ya mmoja, amtaje mke aliyeridhia kushirikiana nae kwenye malezi. Pia Mwanaume ambae hajaoa hataruhusiwa kuwa Mlezi wa kuaminika.

### 2.6.6 Haki za Mlezi wa kuaminika

Mlezi wa kuaminika ana haki zifuatazo:

i. Kupewa ushauri/msaada wa kitaalamu kutoka kwa Afisa Ustawi wa Jamii na wataalamu wengine wanaotoa huduma za Ustawi wa Jamii kwa watoto walio katika mazingira hatarishi ili kumwezesha kutoa malezi stahiki kwa mtoto.
ii. Kupewa taarifa kamili za mtoto ikiwemo asili yake na sababu za mtoto kuwekwa chini ya malezi ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa, afya yake ikiwemo taarifa za chanjo, historia ya elimu na msaada wowote wa kisaikolojia ambao amewahi kupewa na mahitaji mengine ambayo Mlezi wa kuaminika anaweza kumsaidia.
iii. Kufanya maamuzi ya msingi ya kila siku kuhusiana na Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto akiwa chini ya uangalizi wake.
iv. Kuheshimu faragha yake na kutobugudhiwa na Wazazi/Walezi wa mtoto au ndugu wengine wa familia wakati wa kutekeleza jukumu lake la kutoa malezi.

v. Kupewa taarifa na Ofisi ya Ustawi wa Jamii kuhusu jambo au tukio lolote ambalo linaweza kumuathiri mtoto akiwa mikononi mwake au kuathiri watoto wengine ndani ya familia.

vi. Kushirikishwa katika shughuli mbalimbali zinazohusu masuala ya Watoto katika Halmashauri husika.

**2.6.7 Majukumu ya Mlezi wa kuaminika**

a. Kumfundisha mtoto stadi za maisha kulingana na umri wake.

b. Kumpatia mtoto huduma zote za msingi ikiwemo lishe, matibabu, chanjo, mavazi, malazi, kusimamia na kufuatilia maendeleo ya mtoto kielimu.

c. Kushirikiana na Afisa Ustawi wa Jamii kuandaa Mpango wa Huduma kwa ajili ya mtoto na kutathmini maendeleo ya mtoto.

d. Kushirikiana na Afisa Ustawi wa Jamii ili kumuandaa mtoto kumtengamanisha na wazazi /ndugu zake.

e. Kuhakikisha mtoto anahudhuria mahakamani pale ambapo atapaswa kufanya hivyo.

f. Kutoa taarifa kwa Afisa Ustawi wa Jamii iwapo atahitaji kusafiri na mtoto au bila mtoto nje ya Halmashauri.

g. Kutoa taarifa kwa Afisa Ustawi wa Jamii iwapo atahitajika kuhama eneo analoishi, Halmashauri, Mkoa au Nchi, angalau mwezi mmoja kabla ya safari hiyo ili taratibu nyingine zifanyike.

h. Kushirikana na wataalam wa programu ya marekebisho ya tabia na kuhakikisha mtoto anahudhuria programu, yaani kushiriki katika kupanga mpango wa matunzo na mchakato wa mapitio na kufanya kazi na wataalam wa programu katika utekelezaji wa malengo ya mtoto.

i. Kutoa mrejesho kwa Afisa Ustawi wa Jamii juu ya maendeleo ya mtoto katika familia na jamii.

j. Kutoa ushirikiano kwa mtaalamu wa Ustawi wa Jamii anapotembelea mtoto nyumbani.

k. Kuimarisha mahusiano kati ya mtoto na familia/ndugu zake.

l. Kutoa taarifa Ofisi ya Ustawi wa Jamii na kituo cha Polisi ndani ya masaa 24, pale mtoto anapokuwa ametoroka.
m. Kutoa taarifa kwa Afisa Ustawi wa Jamii na ndugu wa mtoto pale ambapo itatokea mtoto amefariki au kupatwa na jambo lolote la dharura.
n. Mlezi wa kuaminika atatakiwa kuwataarifu wana familia kabla ya kupokea mtoto.

**Angalizo:** Mlezi wa kuaminika atatakiwa kuhakikisha anamlea mtoto kama mtoto mwingine aishiye katika familia hiyo.

### 2.6.8 Majukumu ya Afisa Ustawi wa Jamii

a. Kuwatambua na kuwapatia mafunzo Walezi wa kuaminika.
b. Kutoa ushauri wa kitaalam kwa Mlezi wa kuaminika kuhusiana na malezi, matunzo na ulinzi wa mtoto.
c. Kushirikiana na Asasi za Kiraia zilizopo katika eneo husika kuwezesha Walezi wa kuaminika kutekeleza majukumu yao ya malezi kwa ufanisi.
d. Kushirikiana na Asasi zilizopo kuunganisha watoto na huduma mbalimbali kulingana na mahitaji yao.
e. Kushirikiana na Mlezi wa kuaminika katika kuandaa na kufanya mapitio ya Mpango wa Huduma ya Mtoto.
f. Kumtembelea mtoto akiwa chini ya malezi ya Mlezi wa kuaminika kwa mujibu wa kanuni za Mlezi wa kuaminika, kwa utaratibu ufuatao;
    i. Ndani ya siku saba baada ya tarehe ya mtoto kuwekwa kwenye hifadhi ya familia ya kuaminika na mara moja kwa kila baada siku 28 au;
    ii. Mara tu taarifa zozote za unyanyasaji zinapotolewa; na
    iii. Ndani ya wiki moja mara baada ya kupokea taarifa zozote kutoka kwa mtoto, Mlezi wa kuaminika au mtu mwingine yeyote atakayeonyesha uhitaji wa mtoto kutembelewa.
g. Kuandaa taarifa kila baada ya kumtembelea mtoto.
h. Kusitisha malezi ya Mlezi wa kuaminika kutokana na sababu zifuatazo:
    i. Pale ambapo atagundua uwepo wa vitendo vya unyanyasaji na ukatili dhidi ya mtoto.

ii. Pale ambapo atajiridhisha kuwa mtoto anaweza kutengamanishwa na kuunganishwa na wazazi wake au familia.
iii. Pale ambapo atabaini kuwa hifadhi hiyo haina maslahi kwa mtoto.
iv. Pale ambapo anapoteza sifa za kuwa Mlezi wa kuaminika, mfano: kutengana kwa walezi wa kuaminika.
v. Pale mtoto atakapoomba mwenyewe kutaka kutoka kwa kuzingatia umri wa mtoto, uelewa, hali, ukomavu na tathimini ya Afisa Ustawi wa Jamii.
vi. Kufariki kwa Mlezi wa kuaminika.

**Angalizo:**

- Mlezi wa kuaminika hatapewa watoto zaidi ya watatu kwa mara moja isipokuwa kama watoto hao ni ndugu wa familia moja ambao hawapaswi kutenganishwa.
- Mtoto asilazimishwe kuabudu katika dini ambayo Mlezi wa kuaminika anaabudu.

### 2.6.9 Muda wa mtoto kupata malezi kwa Mlezi wa kuaminika

i. Kwa mtoto ambaye ni mhanga wa ukatili, unyanyasaji, udhalilishaji na utelekezaji, Afisa Ustawi wa Jamii wa Halmashauri atafanya tathmini ili kuamua ni kwa muda gani mtoto huyo apatiwe makazi. Hata hivyo, muda huo hautakiwi kuzidi miezi sita isipokuwa tu kama ni kwa maslahi bora ya mtoto. Kwa watoto walio katika mkinzano na sheria na watoto walio katika hatari ya kukinzana na sheria watakaa kwa Mlezi wa kuaminika kwa kipindi ambacho mtoto anashiriki katika mpango wa Marekebisho ya Tabia.
ii. Pale ambapo Mlezi wa kuaminika ataishi na mtoto ambaye amepewa dhamana na mahakama, atamlea mpaka pale mahakama itakapoamua vinginevyo.
iii. Pale ambapo amewekwa chini ya Mlezi wa kuaminika kwa amri ya malezi inayotolewa na mahakama ambayo inaweza kuwa kwa muda wa miaka 3 au hadi pale mtoto atakapofika umri wa miaka 18 au miaka 21.

### 2.6.10 Motisha kwa Mlezi wa kuaminika

Mlezi wa kuaminika halipwi mshahara ila anaweza kupewa motisha kama vile vifaa vya malazi, nguo na vifaa/mahitaji mbalimbali ya msingi yanayohitajika kwa mtoto. Vifaa hivi vitategemea hali halisi ya mazingira ya Mlezi wa kuaminika na upatikanaji wa fedha.

## MADA YA TATU
## HAKI ZA MTOTO

**3.1 Muda wa kuwezesha: Dk 60**

**3.2 Malengo ya Mada**

Ifikapo mwisho wa mada hii washiriki wataweza kuelewa

- Chimbuko la haki za mtoto
- Haki za msingi za mtoto kwa lengo la kuzisimamia
- Wajibu wa mtoto kwa Wazazi/Walezi na Jamii

**3.3 Njia za uwezeshaji**

- Mhadhara mfupi
- Bangua bongo
- Majadiliano katika vikundi
- Majadiliano ya pamoja

**3.4 Hatua za kuwezesha**

**Hatua ya 1:** Toa utangulizi na malengo ya mada.

**Hatua ya 2:** Toa maelezo mafupi kuhusu chimbuko la Haki za Mtoto.

**Hatua ya 3:** Wezesha washiriki kubungua bongo kuhusu; Maana ya Haki za Mtoto, Makundi ya Haki za Mtoto na Wajibu wa Mtoto.

**Hatua ya 4:** Hitimisha kwa maelezo ya ufafanuzi kuzingatia kitabu cha rejea.

**3.5 Maelezo ya Mada**

**3.5.1 Chimbuko la Haki za Mtoto**

Chimbuko la Haki za Mtoto linatokana na Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Mtoto ulioidhinishwa na Nchi Wanachama wa Umoja wa Mataifa mnamo Novemba 20, 1989 na kuridhiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Juni 10, 1991. Mkataba huu unaelekeza Serikali za nchi wanachama kuhakikisha kuwa haki hizi zinatekelezwa na kuheshimiwa.

Kutokana na mkataba wa Kimataifa wa Haki za Mtoto, Umoja wa Nchi Huru za Afrika kwa Umoja wa Afrika ulipitisha Mkataba wa Afrika wa Haki na Ustawi wa Mtoto mwaka wa 1990. Mkataba huo ulilenga kuhakikisha kuwa Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Mtoto unatekelezwa kwa kuzingatia mila, desturi na tamaduni za kiafrika.

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imetia saini mkataba huu ambapo mikataba yote miwili imetoa majukumu kwa Serikali zinazoridhia kulinda na kuendeleza haki za watoto. Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kutekeleza mikataba hiyo, iliandaa Sera ya Maendeleo ya Mtoto 2008 na kutunga Sheria ya Mtoto Na. 21 ya mwaka 2009 iliyofanyiwa marekebisho 2019 na kanuni zake ili kuweza kutekeleza haki hizo.

### 3.5.2 Haki za mtoto zimegawanyika katika makundi makuu matano

**a. Haki ya Kuishi**

Haki hii inalenga katika kuhakikisha kuwa mtoto anazaliwa na anaishi salama kwa;

i. Kumpatia mama mjamzito huduma bora za afya zikiwemo chanjo za kumkinga na magonjwa mbalimbali, kumpa lishe bora na ulinzi dhidi ya ukatili.

ii. Kumpatia mtoto huduma za afya, chanjo na matibabu.

iii. Kumpatia mtoto lishe bora , malazi na mavazi ya kumsitiri kulingana na hali ya hewa.

iv. Kuhakikisha kuwa mtoto anapewa huduma ya uchangamshi wa awali katika umri wa miaka 0 -8.

**b. Haki ya Kuendelezwa**

Haki hii inalenga katika kuhakikisha kuwa mtoto anaendelezwa katika nyanja za kielimu, kimaadili na kiimani. Mchakato huu wa kumuendeleza mtoto katika nyanja hizo unasaidia kuibua ubunifu na maarifa yanayomuwezesha mtoto kukua na kufikia utimilifu wake. Haki hii inajumuisha afua rafiki na stahiki za kumwendeleza mtoto mwenye ulemavu.

**c. Haki ya Kulindwa**

Haki hii inalenga kuimarisha ulinzi wa mtoto akiwemo mtoto mwenye ulemavu dhidi ya vitendo vyote vya ukatili, unyanyasaji, unyonyaji na utelekezaji. Hii ni pamoja na kuboresha mifumo ya kuzuia ukatili na kutoa huduma kwa wahanga wa ukatili dhidi ya watoto.

**d. Haki ya Kushiriki**

Haki hii inalenga kuhakikisha kwamba watoto wanapewa nafasi ya kushiriki na kushirikishwa katika masuala yanayowahusu ikiwa ni pamoja na kutoa maoni, kusikilizwa na kushiriki katika maamuzi mbalimbali katika familia na jamii kwa ujumla. Wazazi/Walezi na Jamii wanatakiwa kuweka mifumo rafiki ya kuwapa nafasi watoto kujieleza na kusikilizwa hasa kwa kuzingatia umri, hali, uelewa na ukomavu wa akili zao.

**e. Haki ya kutobaguliwa**

Haki hii inalenga kuwalinda watoto dhidi ya vitendo vyote vya ubaguzi wa kijinsia, utaifa, rangi, dini, lugha, hali ya kipato, hali zao za ulemavu, afya, mila na desturi na asili yao.

### 3.5.3 Wajibu wa Mtoto

Kila mtoto ana wajibu ufuatao:

i. Kuheshimu na kuwatii Wazazi/Walezi na Wanajamii.
ii. Kufanya kazi nyepesi kulingana na umri wake.
iii. Kuwasaidia wazazi/walezi, watu wazima, wazee na watu wenye ulemavu pale inapohitajika.
iv. Kulinda na kuimarisha mshikamano katika Familia, Jamii na Taifa, ikiwa ni pamoja na kulinda maadili ya jamii ya kitanzania.
v. Kujifunza na kusoma kwa bidii.
vi. Kufanya na kuzingatia usafi binafsi na mazingira yanayomzunguka kutokana na umri na hali ya mtoto.
vii. Kuwalinda na kuwapendaea wale walio wadogo kwao na kuwalinda wenye kuhitaji ulinzi.

**Angalizo:**

- Utekelezaji wa wajibu wa mtoto utazingatia umri, afya, hali ya ulemavu, ukomavu na uwezo wa kiakili wa mtoto katika kutekeleza wajibu huo.
- Utekelezaji wa Haki za Mtoto unapaswa kuzingatia maslahi bora ya mtoto.

# MADA YA NNE
# KANUNI ZA MAADILI ZA KUHUDUMIA WATOTO

## 4.1 Muda wa kuwezesha: Dk 60

## 4.2 Malengo ya Mada

Ifikapo mwisho wa mada hii washiriki wataweza:

- Kuelewa kanuni za maadili za kufanya kazi na watoto
- Kufahamu mambo muhimu ya kuzingatia wakati wa kuwahudumia watoto

## 4.3 Njia za uwezeshaji mada

- Mihadhara mifupi
- Majadiliano katika vikundi vidogo
- Majadiliano ya pamoja

## 4.4 Vifaa vya kuwezesha

- Bango kitita
- Kalamu za wino mzito
- Vitini vya sheria
- Projecta

## 4.5 Hatua za kuwezesha

**Hatua ya 1:** Toa mhadhara mfupi kuhusu Malengo ya Mada.

**Hatua ya 2:** Wagawe washiriki katika vikundi na wafanye yafuatayo;

- Waorodheshe kanuni za maadili za kufanya kazi na watoto.
- Waainishe mambo muhimu ya kuzingatia wakati wa kuwahudumia watoto.

**Hatua ya 3**: Wezesha vikundi kuwasilisha kazi zao.

**Hatua ya 4:** Hitimisha kwa kuelezea kanuni za maadili za kufanya kazi na watoto na mambo muhimu ya kuzingatia wakati wa kuwahudumia watoto.

## 4.6 Maelezo ya Mada

### 4.6.1 Kanuni na maadili ya kufanya kazi na watoto

Katika kuwahudumia watoto, watoa huduma wanapaswa kuzingatia kanuni na maadili ya kufanya kazi na watoto. Kanuni na maadili hayo ni kama ifuatavyo:

**a. Eneo la utoaji Huduma**

i. Kuweka maslahi ya mtoto kwanza wakati wote wa utoaji huduma.

ii. Kutumia maarifa yao kuwaelewa watoto, kutambua na kuthamini vipawa vyao ili kuwasaidia watoto wote wakiwemo watoto walio katika mazingira hatarishi.

iii. Kutoa huduma kwa watoto wote kwa kuzingatia kanuni za maadili za kuwahudumia watoto.

iv. Kutumia lugha rahisi na inayoeleweka kwa watoto wakati wa kutoa huduma.

v. Kuwapa watoto nafasi ya kuuliza na kutafuta ufafanuzi wa maswali yanayowatatiza.

vi. Kupata kibali/ridhaa kutoka kwa mtoto, wazazi, walezi au mamlaka zinazotambulika kisheria kabla ya kurekodi sauti au video ya mtoto.

**b. Utambuzi wa utu na thamani ya Mtoto:**

i. Kuheshimu utu na thamani ya mtoto.

ii. Kumjali na kumheshimu kila mtoto, kwa kuzingatia tofauti za mila na desturi.

iii. Kuwasaidia watoto kutambua na kufafanua malengo yao na kuongeza uwezo wa kushughulikia mahitaji yao wenyewe.

**c. Umuhimu wa uhusiano katika Jamii:**

i. Kutambua na kuelewa kuwa uhusiano chanya baina ya watoto wote ni nyenzo muhimu ya mabadiliko.

ii. Kushirikisha watoto katika kutafuta marafiki ili kukuza, kurejesha, kudumisha, na kuimarisha ustawi wa watoto wote.

**d. Uadilifu:**

i. Kuzingatia usiri na faragha katika kutoa huduma kwa watoto.

ii. Kuepuka kutoa taarifa za siri za mtoto isipokuwa kwa ridhaa/kibali kutoka kwa mtoto mwenyewe, mzazi, mlezi au mtu aliyeidhinishwa kisheria.

**Angalizo:**
**Mambo Muhimu ya Mlezi wa kuaminika kuzingatia wakati anapoishi na mtoto;**

- Kuzingatia maadaili ya kufanya kazi na watoto.
- Kufuatilia mwenendo wa tabia baina ya mtoto na mtoto.
- Kutambua na kuzingatia mahitaji maalum ya watoto husussan watoto wenye ulemavu.
- Kutoa taarifa kwa Afisa Ustawi wa Jamii anapobaini mbadiliko ya tabia ya mtoto.

## MADA YA TANO
## ULINZI NA USALAMA WA MTOTO

**5.1 Muda wa kuwezesha:** Dk 120

### 5.2 Malengo ya Mada

Ifikapo mwisho wa mada hii washiriki wataweza:

- Kutambua watoto wanaohitaji ulinzi na usalama
- Kuelewa hatua za kuchukua pindi itakapobainika kwamba mtoto amefanyiwa au yuko katika hatari ya kufanyiwa ukatili
- Kufahamu aina, viashiria na madhara ya ukatili na unyanyasaji dhidi ya watoto.
- Kuelewa sababu za ukatili dhidi ya watoto
- Kuelewa mamlaka zenye dhamana ya kushughulikia ulinzi na usalama wa mtoto

### 5.3 Njia za uwezeshaji

- Mhadhara mfupiBungua bongo
- Kazi za vikundi
- Majadiliano ya pamoja

### 5.4 Hatua za kuwezesha

**Hatua ya 1:** Toa maelezo mafupi ya utangulizi.

**Hatua ya 2:** Wezesha washiriki kubungua bongo kuhusu aina za watoto wanaohitaji ulinzi na usalama.

**Hatua ya 3:** Wagawe washiriki katika vikundi. Kwa kutumia jedwali lililo kwenye rejea, waongoze wajaze jedwali kwa kuonyesha namna ya kumtambua mtoto aliyefanyiwa unyanyasaji huo na madhara na athari za ukatili na unyanyasaji wa watoto kwa kila aina ya unyanyasaji na ukatili.

**Hatua ya 4**: Wawezeshe washiriki kuwasilisha kazi za vikundi na ongoza mjadala wa pamoja.

**Hatua ya 5**: Ongoza mjadala wa sababu zinazochangia watoto kufanyiwa ukatili na unyanyasaji.

**Hatua ya 6**: Toa mhadhara mfupi juu ya hatua za kuchukua pale mtoto anapobainika kuwa amefanyiwa ukatili au yuko katika hatari ya kufanyiwa ukatili au anayehitaji ulinzi na usalama

**Hatua ya 7**: Toa mhadhara mfupi juu ya mamlaka na wadau wengine wanaoshughulikia masuala ya ulinzi na usalama wa mtoto.

**Hatua ya 8:** Hitimisha mada kwa kutoa muhtasari wa yaliyojadiliwa katika mada hii

## 5.5 Maelezo ya Mada

### 5.5.1 Dhana ya ulinzi na usalama wa mtoto

- **Ulinzi wa mtoto**: Ni shughuli zote zinazolenga kuzuia aina zote za vitendo vya ukatili na unyanyasaji wa mtoto na kutoa huduma kwa watoto waliofanyiwa vitendo vya ukatili na unyanyasaji.
- **Unyanyasaji na ukatili dhidi ya watoto:** Ni vitendo vinavyohusisha ukiukwaji wa haki ya mtoto ambao unasababisha madhara ya kimwili, kimaadili au kifikra ukijumuisha kupigwa, kutukanwa, kubaguliwa, kutelekezwa, kunyanyaswa kijinsia na kazi za kinyonyaji.
- **Aina za watoto wanaohitaji ulinzi na usalama:** Pamoja na watoto waliofanyiwa vitendo vya unyanyasaji na ukatili, watoto wengine wanaohitaji ulinzi na usalama ni watoto ambao wana matatizo ya kijamii kwa mfano watoto waliotelekezwa, watoto ambao wazazi wao ni wagonjwa sana, watoto yatima, watoto wanaojilea, wanaolelewa na walezi wazee wasiokuwa na uwezo, watoto ambao wazazi wana ulemavu wa afya ya akili, watoto wanaolelewa na mtu mwenye ulemavu asiyejiweza, watoto wanao lelewa na wazazi au walezi wenye ugonjwa wa muda mrefu.

### 5.5.2 Aina za unyanyasaji na ukatili dhidi ya watoto

Kuna aina mbalimbali za unyanyasaji dhidi ya watoto, ikiwa ni pamoja na;

i. Unyanyasaji wa kimwili.
ii. Unyanyasaji wa kukatwa viungo.
iii. Unyanyasaji wa kihisia.
iv. Ukatili na unyanyasaji wa watoto mtandaoni.

v. Utelekezaji.

vi. Unyanyasaji wa kingono na unyonywaji.

vii. Usafirishaji haramu wa watoto.

viii. Ukeketaji.

ix. Utumikishwaji wa watoto.

**Jedwali Na 2: Namna ya kumtambua mtoto aliyefanyiwa unyanyasaji na ukatili, madhara na huduma anazopaswa kupatiwa**

| Na. | Aina za unyanyasaji na tafsiri zake | Namna ya kutambua mtoto aliyefanyiwa unyanyasaji huo | Madhara na athari za ukatili na unyanyasaji wa watoto | Jinsi ya kumsaidia kwa mtoto aliyefanyiwa ukatili |
|---|---|---|---|---|
| 1. | **Unyanyasaji wa kimwili** Kumpiga, kumtikisa, kumrusha, kumpa sumu, kumuunguza, kumzamisha kwenye kimiminika, kumziba pumzi au vinginevyo vinavyomsababishia mtoto madhara kwenye mwili au hata kuugua na kuathirika kiafya. Hii inahusisha pia kushindwa kumlinda mtoto dhidi ya matendo hayo.<br>• Husababisha majeraha mwilini. | Mtoto kuwa na majeraha yanayosababishwa na ukatili.<br>• Majeraha yenye chanzo chenye utata.<br>• Mabadiliko ya kitabia kwa mtoto; kama hasira, chuki, woga au wasiwasi na kukosa furaha.<br>• Mtoto kushindwa kujieleza vizuri. | Ulemavu, kifo, magonjwa ya akili, makovu na msongo wa mawazo | • Huduma ya matibabu.<br>• Msaada wa kisheria.<br>• Msaada wa Afya ya Akili, Kisaikolojia na Kijamii.<br>• Marekebisho (kwa mtoto aliyepata ulemavu).<br>• Hifadhi ya muda. |
| 2. | **Unyanyasaji wa** | Kukosa | Msongo wa | • Msaada wa |

| Na. | Aina za unyanyasaji na tafsiri zake | Namna ya kutambua mtoto aliyefanyiwa unyanyasaji huo | Madhara na athari za ukatili na unyanyasaji wa watoto | Jinsi ya kumsaidia kwa mtoto aliyefanyiwa ukatili |
|---|---|---|---|---|
| | **kihisia**<br>Ni vitendo vinavyomsababishia mtoto maumivu ya kihisia kama vile kumtukana, kumsimanga, kumsingizia, kumnyanyapaa, kumdhalilisha. Hii inachangia kwa kiasi kikubwa katika kudumaza ukuaji na maendeleo ya mtoto. | uchangamfu, kuwa na woga/hofu, mabadiliko ya tabia, lugha zisizokubalika (mfano matusi), tabia ya kujitenga, kukojoa kitandani, kurudi nyuma kimaendeleo shuleni na kutojiamini. | mawazo, Matatizo ya Afya ya Akili, kutofanya vizuri darasani, kujidhuru mwenyewe au kuwadhuru wengine na hata kifo | Afya ya Akili, Kisaikolojia na Kijamii.<br>• Msaada wa kisheria.<br>• Hifadhi ya muda. |
| 3. | **Utelekezaji**<br>Ni kitendo cha Mzazi/Mlezi kutokutoa huduma stahiki kwa watoto kwa makusudi. | Kudhoofika kwa afya ya mtoto/kuugua mara kwa mara, mtoto kuonekana mchafu (upele, funza na mapunye), kutokuwa mchangamfu na mavazi duni. | Watoto kujiingiza kwenye tabia zisizofaa (ulevi, matumizi ya dawa za kulevya, ukabaji, tabia za ngono, magonjwa, mimba za utotoni, ajira za utotoni, watoto kuondoka kwenye familia na kuingia mitaani, watoto kulelewa kwenye makao | • Hifadhi ya muda.<br>• Mlezi.<br>• Msaada wa Afya ya Akili, Kisaikolojia na Kijamii.<br>• Huduma ya matibabu.<br>• Mahitaji ya muda (chakula, mavazi).<br>• Msaada wa kisheria.<br>• Kuwasiliana na wazazi au walezi waliotelekeza watoto ili kufanya mazungumzo na ili waweze kutoa huduma |

| Na. | Aina za unyanyasaji na tafsiri zake | Namna ya kutambua mtoto aliyefanyiwa unyanyasaji huo | Madhara na athari za ukatili na unyanyasaji wa watoto | Jinsi ya kumsaidia kwa mtoto aliyefanyiwa ukatili |
|---|---|---|---|---|
| | | | | stahiki kwa watoto. |
| 4. | **Unyanyasaji wa kingono**<br>Ni hali ya kutishia kuingilia au kuingilia faragha ya mwili wa mtoto, ikiwa ni pamoja na kuamsha hisia za kujamiiana, kutishia kujamiiana au kujamiiana.<br>Ni pamoja na kushawishi au kumlazimisha mtoto ili ashiriki katika vitendo vyovyote vya ngono, utumiaji wa watoto kufanya ukahaba au kuona au kupiga picha za ngono na kutengeneza vifaa vinavyohusika na ngono | Majeraha sehemu za siri, kutokwa damu sehemu za siri, maambukizi ya magonjwa ya ngono), kutembea kunakoashiria maumivu ya sehemu za siri, kuonyesha tabia za kingono zisizoendana na umri wake (mfano tabia zenye ushawishi wa kingono), matatizo ya kitabia kama vile kuwa na hasira na tabia zisizo za kawaida kama kukataa shule, utoro shuleni, kukojoa kitandani, kuweweseka, kuogopa watu wa jinsi tofauti na yake | Maambukizi ya magonjwa mfano; UKIMWI, kaswende, kisonono, mimba za utotoni, kifo, msongo wa mawazo na ugumba. | • Huduma ya matibabu.<br>• Msaada wa kisheria.<br>• Msaada wa Afya ya Akili, Kisaikolojia na Kijamii.<br>• Hifadhi ya muda. |
| 5. | **Usafirishaji haramu wa watoto**<br>Ni kitendo cha kumsafirisha mtoto kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine kwa madhumuni ya kumtumikisha au kumfanyia vitendo | Mahusiano duni baina ya mtoto na yule anayemsafirisha, hofu ya mtoto anayesafirishwa, kutokuhudhuria shule, kufanyishwa kazi | Utumikishwaji wa watoto, kudumaza maendeleo ya mtoto na kukatisha matarajio yake ya baadae ikiwemo kukosa haki ya | • Hifadhi ya muda.<br>• Msaada wa kisheria.<br>• Msaada wa Afya ya Akili, Kisaikolojia na Kijamii.<br>• Huduma ya |

| Na. | Aina za unyanyasaji na tafsiri zake | Namna ya kutambua mtoto aliyefanyiwa unyanyasaji huo | Madhara na athari za ukatili na unyanyasaji wa watoto | Jinsi ya kumsaidia kwa mtoto aliyefanyiwa ukatili |
|---|---|---|---|---|
| | vya unyonyaji. Vitendo hivyo mara nyingi huambatana na ushawishi na ahadi za uongo na ujira mdogo. | za kinyonyaji mfano biashara ya ngono, utumikishwaji katika migodi, mashamba na kazi za nyumbani na sehemu za starehe pamoja na Afya duni. | elimu, matibabu na kutelekezwa. | matibabu.<br>• Kuunganishwa na familia. |
| 6. | **Utumikishaji wa watoto**<br>Ni kitendo cha kumfanyisha mtoto kazi bila ujira au kwa ujira mdogo ambazo hazilingani na umri wake na zinaathiri maendeleo yake kimwili na kiakili. | Mtoto kufanyishwa kazi inayodhuru na kuathiri afya yake, kufanya kazi zaidi ya saa sita kwa siku, kufanya kazi ambayo hailingani na umri wake, kufanya kazi bila malipo au kwa malipo pungufu, kutoenda shule, kudumaa, kuhusishwa katika kuuza biashara ndogondogo ikiwemo karanga, barafu (*ice cream*) matunda n.k | Magonjwa, ulemavu, udumavu, majeraha na makovu, afya kudhoofika, kuathirika kisaikolojia (mfano kuwa na hofu na kutokujiamini), kifo, mtoto kujiingiza katika mazingira hatarishi, kuwa katika hatari ya kufanyiwa vitendo vya ngono au kufanyiwa vitendo vya ngono. | • Msaada wa kisheria.<br>• Hifadhi ya muda.<br>• Msaada wa Afya ya Akili, Kisaikolojia na Kijamii.<br>• Huduma ya matibabu.<br>• Huduma ya elimu. |
| 7. | **Ukatili wa watoto mtandaoni**<br>Ni ukatili wanaofanyiwa watoto kupitia mitandao ya kijamii ikiwemo whatsapp, instagram, Face | • Muda mwingi hutumia mitandao ya kijamii kwa njia za kificho.<br>• Kujitenga na kukaa sehemu | • Kushuka kitaaluma.<br>• Huzuni au kulia.<br>• Anakuwa mwoga na kutojiamini. | • Msaada wa kisheria.<br>• Msaada wa Afya ya Akili, Kisaikolojia na Kijamii.<br>• Huduma ya |

| Na. | Aina za unyanyasaji na tafsiri zake | Namna ya kutambua mtoto aliyefanyiwa unyanyasaji huo | Madhara na athari za ukatili na unyanyasaji wa watoto | Jinsi ya kumsaidia kwa mtoto aliyefanyiwa ukatili |
|---|---|---|---|---|
| | book. Ukatili huo unahusisha mawasiliano yanayohusu ujumbe wa kingono au kushawishiwa kupiga picha za utupu au kujirekodi na kutuma kwa watuhumiwa. | za faragha.<br>• Wanakuwa wajeuri.<br>• Hapendi kujihusisha na shughuli mbalimbali katika familia.<br>• Kushuka kitaaluma.<br>• Anakuwa na huzuni au kulia.<br>• Anakuwa mwoga na kutojiamini. | • Ni rahisi kufanyiwa ukatili wa kingono au kufanyia watoto wengine ukatili wa kingono.<br>• Inaharibu mahusiano yake na jamii.<br>• Inaweza kupelekea mtoto akajiua. | matibabu. |

### 5.5.3 Sababu zinazochangia unyanyasaji na ukatili kwa watoto

i. Wazazi/Walezi kutokuwa na mbinu bora za malezi ya watoto, ikiwa ni pamoja na malezi ya kikatili.

ii. Mila na desturi zenye madhara.

iii. Kutokuwepo kwa mahusiano ya karibu kati ya Mzazi/Mlezi na Mtoto.

iv. Mtoto kulelewa na mzazi mmoja bila kupata usaidizi toka kwa mzazi mwingine.

v. Kifo cha Mzazi/Mlezi.

vi. Migogoro/ kuvunjika kwa ndoa.

vii. Mtoto au familia kutengwa na jamii.

viii. Ulevi uliokithiri na matumizi ya madawa ya kulevya.

ix. Imani za kishirikina.

x. Kutowajibika ipasavyo kwa baadhi ya wataalam wanaoshughulikia masuala ya ulinzi na usalama wa mtoto.

xi. Kumomonyoka kwa maadili.

xii. Watoto kutokuwa na makazi maalum (mfano; watoto kuishi na kufanya kazi mitaani).

xiii. Unyanyapaa.

xiv. Watoto kulelewa katika Taasisi (mfano; makao ya watoto, mahabusu za watoto).

xv. Historia ya unyanyasaji na ukatili kwa Mtoto au Mzazi/Mlezi.

xvi. Hali ya ulemavu.

### 5.5.4 Hatua za kuchukua pale mtoto anapobainika kuwa amefanyiwa ukatili au yuko katika hatari ya kufanyiwa ukatili

i. Toa taarifa haraka kwa Afisa Ustawi wa Jamii, Viongozi wa Serikali, Polisi au Mjumbe wa Kamati ya Ulinzi wa Wanawake na Watoto katika eneo husika.

ii. Mpeleke mtoto kwenye kituo cha kutolea huduma kulingana na madhara ya ukatili yaliyomkuta. Hii inaweza kuhusisha kumpeleka mtoto Hospitali au Kituo cha Afya kama mtoto amepata madhara kiafya.

iii. Imarisha ulinzi na ukaribu kwa mtoto ili kupunguza madhara ya ukatili aliofanyiwa.

iv. Toa ushirikiano kwa watendaji wa serikali na wadau katika kuhakikisha ulinzi na ustawi wa mtoto.

v. Kumpatia mtoto hifadhi ya muda kulingana na ukatili aliofanyiwa.

vi. Kumpatia huduma endelevu ya Afya ya Akili na msaada wa Kisaikolojia na Kijamii.

vii. Kumpatia rufaa mtoto kwa taasisi nyingine kulingana na aina ya ukatili aliofanyiwa.

### 5.5.5 Mamlaka zenye dhamana ya kushughulikia ulinzi na usalama wa mtoto

Kwa mujibu wa Sheria ya Mtoto namba 21 ya mwaka 2009 na miongozo mbalimbali, mamlaka zifuatazo zina wajibu na majukumu ya kusimamia ulinzi na usalama wa mtoto:

i. Ofisi ya Kijiji/Mtaa.

ii. Ofisi ya Mtendaji wa Kata.

iii. Polisi.
iv. Mahakama.
v. Vituo vya Afya na Zahanati.
vi. Halmashauri ya Wilaya/Mji/Manispaa/Jiji (Ofisi za Ustawi wa Jamii).

### 5.5.6 Wadau muhimu ambao wanawajibika katika kushughulikia masuala ya ulinzi na usalama wa mtoto

i. Afisa Ustawi wa Jamii
ii. Afisa Maendeleo ya Jamii
iii. Afisa Elimu
iv. Walimu wa malezi
v. Vituo vya kulelea watoto wadogo mchana
vi. Daktari
vii. Afisa Biashara
viii. Afisa Utamaduni
ix. Afisa Habari
x. Afisa Lishe
xi. Hakimu
xii. Mwendesha Mashtaka
xiii. Kamati za Watu Wenye Ulemavu
xiv. Mashirika na Asasi za Kiraia
xv. Taasisi za Kidini
xvi. Wawezeshaji haki jamii
xvii. Wasaidizi wa Ustawi wa Jamii
xviii. Kamati za ulinzi wa wanawake na watoto za Vijiji/Mtaa, Kata na Halmashauri

## MADA YA SITA
## MALEZI, MAKUZI NA MAENDELEO YA AWALI YA MTOTO

### 6.1 Muda wa kuwezesha: Dk 120

### 6.2 Malengo ya Mada

Ifikapo mwisho wa mada hii washiriki wataweza:

- Kuelewa maana ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto
- Kuelewa huduma muhimu za Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto kulingana na umri wa mtoto
- Kutambua wadau ambao wanatoa huduma za Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto

### 6.3 Njia za uwezeshaji

- Mhadhara mfupi
- Bungua bongo
- Kazi za vikundi
- Majadiliano ya pamoja

### 6.4 Hatua za kuwezesha

**Hatua ya 1:** Toa maelezo mafupi ya utangulizi wa mada.

**Hatua ya 2:** Ongoza washiriki kubungua bongo kuhusu maana ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto.

**Hatua ya 3**: Wagawe washiriki katika vikundi wajadili mambo yafuatao:

- Hatua za ukuaji wa mtoto.
- Huduma muhimu katika Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto.

**Hatua ya 4:** Wawezeshe washiriki kuwasilisha kazi za vikundi na kufanya majadiliano ya pamoja kisha toa ufafanuzi.

**Hatua ya 5**: Ongoza washiriki kubungua bongo kuhusu wadau na taasisi ambapo huduma za Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto zinapatikana.

**Hatua ya 6:** Hitimisha kwa kufanya ufafanuzi.

### 6.5 Maelezo ya Mada

#### 6.5.1 Maendeleo ya Mtoto

Ni mchakato wa mabadiliko ambao mtoto anaweza kujitawala kimwili, kiakili, kihisia na uwezo wa kipaji katika kumwendeleza katika kila nyanja na kumwezesha kukabiliana na mazingira. Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto ni huduma zote anazostahili kupewa mtoto mdogo (miaka 0-8) ili kumwezesha kukua na kufikia utimilifu wake katika nyanja zote za kimwili, kiakili, kijamii, kihisia, kimaadili, kimaono na baadaye kushiriki kikamilifu katika ujenzi wa Taifa na kumudu mazingira yake.

#### 6.5.2 Hatua za Ukuaji wa Mtoto

a. **Ukuaji wa Mtoto Kiakili:**

   Kukua kiakili ni kuongezeka kwa uwezo wa kuelewa, kujifunza, kutafakari, kufikiri, kuhusisha, kupanga, kutumia lugha, kutathmini na kujenga taswira. Akili ya mtoto hukua kwa kiwango cha 80% katika kipindi cha kati ya miaka 0 mpaka 3. Matendo ya uchangamshi yatakayochochea ukuaji wa mtoto kiakili ni pamoja na kumpatia lishe, mavazi, malazi, ulinzi na kuwa karibu naye, kujibu maswali yake kwa ufasaha, kumpa vifaa vya michezo na fursa ya kucheza pamoja na wenzake.

b. **Ukuaji wa Mtoto Kimwili:**

   Ukuaji wa mtoto kimwili ni kuongezeka kimaumbile ambako kunaambatana na mabadiliko na ongezeko la urefu, uzito, upana wa mwili na uzito wa ubongo. Mabadiliko ya ukuaji hujitokeza haraka katika miezi 24 ya kwanza. Mabadiliko yanayojitokeza kwa haraka kwa mtoto ni ukuaji wa maungo ya mwili ambayo huenda sambamba na uwezo wake wa kutumia viungo hivyo. Katika mwezi wa kwanza mtoto hana uwezo mkubwa sana wa kutumia viungo vyake. Kadri anavyokua uwezo wa kutumia viungo vyake huongezeka sambamba na umri alionao. Ili mtoto aonyeshe mabadiliko ya ukuaji kimwili kwa wakati unaofaa anahitaji apate mahitaji muhimu. Mahitaji hayo ni pamoja na uangalizi mzuri, mazingira safi na salama na ya kusisimua, michezo na vifaa vya kuchezea. Pia

mtoto anahitaji kuelekezwa katika vitendo mbalimbali vya ukuaji kwa mfano, kukaa, kutembea, kutambaa na kuzungumza.

c. **Ukuaji wa Mtoto Kihisia na Kimaadili:**

i. **Kimaadili:**

Kukua kimaadili ni kujenga uwezo wa mtoto kutambua mambo mazuri katika mazingira anayoishi na kuyafuata. Mambo haya hudhihirishwa kwa vitendo na tabia ya mtoto. Mtoto anaweza kujifunza maadili hayo kwa njia ya hadithi, nyimbo, mila na desturi, vitendawili na taratibu mbalimbali za familia. IIi mtoto aweze kukua kimaadili, anahitaji mazingira mazuri yanayomwezesha kujifunza kwa kuiga na kupokea miongozo na tamaduni nzuri katika jamii husika.

ii. **Kihisia:**

Kukua kihisia kwa mtoto ni kujenga uwezo wa mtoto kuelewa hisia zake na kujifunza namna ya kuzielekeza. Mtoto anaweza kuonyesha hisia kutokana na sababu mbalimbali kwa mfano, furaha anapofanyiwa jambo la furaha au huzuni inapotokea jambo lisilomfurahisha.

**d. Ukuaji Kijamii:**

Kukua kijamii kunamaanisha kuongezeka kwa uwezo wa mtoto kushiriki vizuri katika michezo mbalimbali na wenzake pamoja na shughuli katika familia na jamii. IIi mtoto akue kijamii anahitaji:

i. Kupendwa.
ii. Kuthaminiwa.
iii. Kujengewa uwezo wa kujiamini.
iv. Kushirikishwa katika maamuzi mbalimbali.
v. Kupewa nafasi ya kusikilizwa.
vi. Kuheshimiwa kwa mawazo yake.
vii. Kuelimishwa juu ya haki na wajibu wake.
viii. Kupatiwa miongozo ya tabia, mienendo na matarajio yake toka kwa jamii kulingana na umri wake.

### 6.5.3 Huduma muhimu za Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto (MMMAM)

Mtoto huwa na mahitaji tofauti katika umri tofauti. Mahitaji haya hupelekea mtoto kuhitaji huduma tofauti kulingana na umri wake. Huduma zinazohusiana moja kwa moja na MMMAM ni za Afya, lishe, ulinzi, malezi, uchangamshi wa awali na elimu. Huduma hizi zinatakiwa zitolewe kwa ujumla wake kwa kuzingatia muda na umri stahiki ili kuweza kuleta matokeo yanayotarajiwa.

i. **Huduma za Afya**

Huduma za Afya zinajumuisha matibabu, chanjo na ushauri wa kitalaam kuhusu Afya ya Mtoto. Huduma hii humpa mtoto afya njema kwa kuzuia na kumwepusha mtoto na magojwa ya kuambukiza na kutougua mara kwa mara. Mtoto asipopata huduma hizo anaweza kupata madhara yafuatayo ikiwemo; Vifo, ulemavu, magonjwa ya mara kwa mara, magonjwa ya mlipuko n.k

ii. **Huduma ya lishe**

Lishe inajumuisha upatikanaji wa chakula cha kutosheleza mahitaji na ulishaji, ushauri kuhusu lishe pamoja na upimaji wa maendeleo ya mtoto hasa walio chini ya umri miaka 5. Lishe inazingatia umri wa mtoto na virutubisho muhimu ili kusaidia uimarishaji na ukuaji wa ubongo na viungo vya mwili wa mtoto. Ni muhimu watoto chini ya miaka 5 wapelekwe kliniki ili wapewe ushauri wa kitaalamu kuhusu lishe ili kusaidia ukuaji bora. Ni muhimu kufahamu kuwa ukosefu wa lishe unasababisha madhara yafuatayo: Ulemavu, udumavu wa akili na mwili, magonjwa ya mara kwa mara, ukondefu, utapiamlo, upungufu wa damu, matatizo ya macho, uvimbe wa tezi la shingo na vifo.

iii. **Huduma za uchangamshi wa awali**

Uchangamshi wa Awali wa watoto ni jumla ya matendo yote anayopaswa kufanyiwa mtoto ili awaze kukua vyema na kufikia utimilifu wake. Huduma hii ni muhimu na ya kuzingatia kwa watoto wa umri wa miaka 0 hadi 8. Uchangamshi wa awali unahusisha vitendo vyote chanya wanavyofanya walezi kwa lengo la kumpa mtoto upendo na kujihisi kuthaminiwa. Huduma hii ya

malezi pia huimarisha mawasiliano na mahusiano ya mtoto na wanafamilia au jamii na kusaidia ukuaji mzuri wa ubongo na hisia.

**6.5.4 Uchangamshi wa awali unahusisha mambo yafuatayo:**

i. Kumjenga mtoto kihisia na kitabia. Mzazi/Mlezi anatakiwa kuwa karibu na mtoto, kumwonyesha upendo, kumthamini, kumjengea uwezo wa kujiamini, kumpa nafasi ya kusikilizwa, kuheshimu mawazo yake, kumuelimisha haki na wajibu wake pia kumlea mtoto kulingana na maadili mema ya familia na jamii husika.

ii. Kuandaa mazingira wezeshi ya michezo pamoja na vifaa vya michezo na kujifunzia.

iii. Kumpa mtoto nafasi ya kushiriki katika shughuli za kifamilia na kundi rika hususani nafasi ya kucheza, kufanya shughuli ndogondogo kulingana na umri wake ili mtoto kujenga mahusiano na wanafamilia na watu wengine katika jamii.

iv. Kumjengea mtoto uwezo wa kujitambua na kutambua nafasi yake katika familia, imani ya kidini na kupewa nafasi ya kufanya vitu yeye mwenyewe kwa kuongozwa na Mzazi/Mlezi.

v. Kumpa mtoto fursa ya kujifanyia mambo anayoweza akiwa chini ya uangalizi mfano usafi, kazi za shuleni, kusali na kula ili aweze kujitegemea.

vi. Kutimiza mahitaji ya msingi ya maisha kwa mtoto kama chakula, mavazi, malazi, ulinzi na kufanya ufuatiliaji wa karibu wa mambo yote yanayomuhusu mtoto, pia kutimiza wajibu wa mzazi au mlezi kwa mtoto ipasavyo.

**6.5.5 Uchangamshi wa awali unapaswa kufanywa na Mzazi/Mlezi kwa kutenda vitendo vilivyokusudiwa na kwa kujirudia kwa kuzingatia umri wa mtoto kama ifuatavyo:**

i. **Kabla ya Kuzaliwa**: Mama mzazi wakati wa ujauzito anatakiwa kuwa na afya njema kwa kupata chanjo zote muhimu zitakazomkinga mtoto na magonjwa yatakayoathiri ukuaji wa mtoto akiwa bado tumboni. Mama pia anatakiwa kupata lishe inayofaa yenye viinilishe muhimu ikiwemo vyakula vyenye madini ya joto. Kuna uhusiano mkubwa wa chakula anachokula mama wakati wa

ujauzito na makuzi ya mtoto anapokuwa tumboni. Mama mjamzito anatakiwa pia kuwa na utulivu wa afya ya akili kwani kutokuwa na utulivu kunaweza kuathiri makuzi na maendeleo ya mtoto tumboni na baada ya kuzaliwa.

ii. **Baada ya kuzaliwa**: Mtoto anahitaji kunyonya maziwa ya mama miezi 6 mfululizo bila kuchanganyiwa na kitu chochote na baadae apate chakula kinachofaa kulingana na umri wake na apatiwe uchangamshi kwa kuitikia hisia mbalimbali za mtoto. Pia anatakiwa kupewa matone ya vitamin A, dawa za minyoo na chanjo zote za kukinga magonjwa ya milipuko ikiwemo kifadulo, kupooza, surua, pepo punda, kuhara, donda koo, homa ya ini n.k.

iii. **Miaka 2 hadi 4:** Watoto waendelee kupata huduma zote muhimu kama chanjo, lishe na huduma za uchangamshi kulingana na mahitaji ya ukuaji kimwili, kiakili na kihisia. Katika kipindi hiki Mzazi au Mlezi amwandikishe mtoto katika kituo cha kulelea watoto wadogo mchana ili kupata huduma ya uchangamshi wa awali ambayo inahitajika kusaidia kuimarisha uwezo wa mtoto kubuni na kuongeza umakini wakati wa makuzi yake. Katika umri huu mtoto anakuwa bado ana misamiati michache ya lugha. Hivyo Mzazi/Mlezi unapaswa kumsaidia mtoto kukuza lugha yake kupitia njia ya michezo, nyimbo na hadithi na kuongea naye mara kwa mara. Ni muhimu kutambua kwamba lugha inamsaidia mtoto katika maeneo mengine.

iv. **Miaka 5 hadi 6**: Katika umri huu mtoto atahitajika kujiunga na Shule ya Awali na baadae kujiunga na Elimu ya Msingi. Msisitizo mkubwa katika kipindi hiki ni kuhakikisha kuwa mtoto anapata lishe inayofaa na ya kutosha kwa ajili ya kumsaidia aweze kukua kadri ya umri wake.

v. **Miaka 6 hadi 8:** Katika umri huu mtoto ataendelea kupata lishe, maelekezo na mafunzo yanayohusu maadili kutoka kwa wazazi, elimu na huduma za afya.

### 6.5.6 Wadau na taasisi ambapo huduma muhimu zinapatikana

i. **Huduma za Afya**: Kliniki za Watoto, Zahanati, Vituo vya Afya na Hospitali.

ii. **Huduma za Lishe**: Kliniki za watoto, wataalam wa lishe katika Kata, Wilaya na Hospitali.

iii. **Huduma za Elimu**: Shule za Awali, Shule za Msingi.

iv. **Huduma za Malezi**: Vituo vya kulelea watoto wadogo na wachanga mchana, vituo vya kijamii vya kulelea watoto wadogo mchana, Walezi/Wazazi, familia, vikundi vya kijamii vya malezi chanya na kona za michezo changamshi.

v. **Huduma za Ulinzi**: Wataalam wanaoshughulikia masuala ya ulinzi na usalama wa mtoto mfano; Kamati za Ulinzi wa Mtoto na Mwanamke, Maafisa Ustawi wa Jamii, Dawati la Polisi la Jinsia na Watoto na Vituo vya kutoa huduma za mkono kwa mkono.

| **Angalizo:**<br>Mzazi/Mlezi anapaswa kufahamu kuwa huduma za Uchangamshi wa Awali ni za msingi katika kumlinda mtoto dhidi ya vitendo vyote vya ukatili, unyanyasaji, unyonyaji na utelekezaji. |
|---|

## MADA YA SABA
## AFYA YA AKILI NA MSAADA WA KISAIKOLOJIA NA KIJAMII

**7.1 Muda wa kuwezesha:** Dk 120

### 7.2 Malengo ya Mada

Ifikapo mwisho wa mada, washiriki wataweza:

- Kueleza maana ya Mahitaji ya Kisaikolojia na Kijamii (Psycho Social Support-PSS)
- Kutaja mahitaji muhimu ya kisaikolojia na kijamii ya watoto walio katika mazingira hatarishi
- Kueleza umuhimu wa Mahitaji ya Kisaikolojia na Kijamii kwa watoto walio katika mazingira hatarishi
- Kutaja athari za ukosefu wa Mahitaji ya Kisaikolojia na Kijamii kwa watoto walio katika mazingira hatarishi
- Kutaja athari za ukosefu wa Mahitaji ya Kisaikolojia na Kijamii kwa watoto walio katika mazingira hatarishi kwa jamii

### 7.3 Njia za uwezeshaji

- Mhadhara mfupi
- Bungua bongo
- Majadiliano ya vikundi
- Majadiliano ya pamoja
- Tafakari ya kuongozwa

### 7.4 Hatua za kuwezesha

**Hatua ya 1**: Toa maelezo mafupi ya utangulizi wa mada.

**Hatua ya 2**: Wezesha washiriki kufanya tafakari ya kuongozwa juu ya hali au tukio fulani ambalo lilitokea katika maisha yao au ya mtu wanayemfahamu.

**Hatua ya 3:** Wezesha washiriki kubungua bongo juu ya mahitaji muhimu ya kisaikolojia ya watoto walio katika mazingira hatarishi, mahitaji yote yatakayoibuliwa yaandikwe kwa ufupi ubaoni/kwenye bango kitita.

**Hatua ya 4**: Ongoza washiriki kupata tafsiri inayokubalika ya Mahitaji ya Kisaikolojia na Kijamii na baada ya hapo bainisha ni yapi mahitaji ya ukweli ya kisaikolojia na kijamii kwa kurejea mahitaji yaliyoandikwa ubaoni/kwenye bango kitita.

**Hatua ya 5**: Wezesha washiriki wajigawe kwenye vikundi na wajadili:

- Mahitaji mbalimbali ya kisaikolojia na kijamii ya watoto walio katika mazingira hatarishi katika eneo lao, jinsi yanavyotekelezwa na njia bora zaidi za kuwasaidia.
- Madhara na athari za ukosefu wa mahitaji ya kisaikolojia na kijamii kwa watoto walio katika mazingira hatarishi na kwa jamii.

**Hatua ya 6**: Wezesha vikundi kuwasilisha kazi zao na kufanya majadiliano ya pamoja.

**Hatua ya 7:** Jazia mapungufu na kuongoza washiriki kuyaibua na kuyajadili.

**Hatua ya 8:** Hitimisha kwa kujazia mapungufu na kukazia umuhimu wa kutoa mahitaji ya kisaikolojia na ya kijamii kwa watoto walio katika mazingira hatarishi kwa kuzingatia tofauti na hali zao.

## 7.5 Maelezo ya Mada

Huduma ya msaada wa kisaikolojia na kijamiii inalenga kuimarisha uwezo wa mtu kijamii, kiakili, kihisia na kiroho katika kukabiliana na hisia hasi zinazotokana na msongo unaosababishwa na matukio na migogoro kama kifo, msiba, ugonjwa na vitendo vya ukatili. Huduma hii inalenga katika kuzuia na kuponya msongo wa mawazo na inamgusa mtu na mazingira anapoishi.

### 7.5.1 Mahitaji ya kisaikolojia na kijamii

**a. Upendo**

Upendo ni muhimu kwa maisha ya kila binadamu. Hivyo watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi nao wanahitaji kupendwa na Wazazi/Walezi na jamii. Upendo wa Mzazi au Mlezi ndio msingi wa malezi bora ya mtoto. Ni muhimu Wazazi, Walezi na jamii nzima kutambua kuwa:

i. Mtoto hujifunza kupenda kutokana na anavyopendwa na kuona vitendo vya upendo kutoka kwa watu wanaomzunguka.

ii. Mtoto anahitaji sana upendo hasa akiwa na changamoto.

iii. Upendo kati ya Wazazi au Walezi, huwawezesha watoto wao kujipenda na kuwapenda watu wengine.
iv. Upendo ni lazima utamkwe na kutendwa kama hautamkwi na kutendwa siyo upendo. Vitu hivi viwili vinategemeana.
v. Kama upendo wa kweli haupo nyumbani, watoto watatafuta njia mbadala kujifunza upendo, mathalani kutoka kwenye magazeti au picha na vitu vingine ambavyo si vyanzo vizuri vya upendo.
vi. Upendo hujenga kuaminiana.
vii. Upendo ni kushirikiana mambo yote.
viii. Upendo hujali watu kuliko vitu.
ix. Upendo ni kutoa muda wako kwa ajili ya watu wengine.
x. Upendo ni kusikiliza neno lolote au kitendo chochote kinachoweza kumfanya binadamu ajisikie kupenda au kupendwa.

**Angalizo:**
Kuwapenda watoto walio katika mazingira hatarishi huwaondolea unyonge na tabia ya kujitenga. Tuwakubali kama walivyo.

**b. Kutambuliwa**

Watoto walio katika mazingira hatarishi wanahitaji kujisikia na kuona kwamba walezi na jamii wanatambua kuwepo kwao. Ni muhimu kwa Mlezi au Mzazi kukumbuka kwamba kila binadamu ni wa pekee na kila mtoto ni muhimu. Tunapaswa kutambua umuhimu na upekee wa kila mtoto.

Mtoto anaweza kujitambua na kujiamini hasa kwa kuona wazazi au walezi wakijiheshimu, kujitunza na kumshirikisha. Kwa watoto wadogo:

i. Unapomruhusu kusaidia katika shughuli ndogondogo na kutambulishwa kwa wageni, huanza kujifunza na kujiamini.
ii. Kumruhusu mtoto kujibu maswali anapoulizwa kwani kwa kufanya hivyo humjengea mtoto kujiamini na kuweza kujieleza. Mara nyingi, wazazi au walezi hupenda kuwajibia hii inawafanya Watoto wasijiamini.
iii. Kuwapa watoto nafasi ya kuamua mambo yanayowahusu kama vile mavazi na mambo mengine ingawaje maamuzi ya mwisho yanaweza kuwa ya

Wazazi au Walezi. Kumshirikisha mtoto katika kuamua husaidia kumjenga mtoto kimaamuzi.

iv. Kupata nafasi ya kukaa na watoto na kuwasikiliza.

v. Kumwamini mtoto na kumpa majukumu ambayo yanaweza kuonyesha kuwa unamwamini au anaaminika. Hii itamwezesha mtoto kujipenda.

c. **Kuwafanya Watoto kuwa salama**

Usalama ni hitaji muhimu lenye mawanda mapana sana. Ipo mifano tofauti inayogusa fikra za watoto juu ya usalama wao hata wakiwa na walezi ambayo ni pamoja na;

i. Wazazi au walezi wanapogombana watoto hupatwa na wasiwasi.

ii. Wazazi wanapoweza kutafuta njia za kuelewana kwa upendo na amani huwawezesha watoto kuelewa kwamba kutoelewana kupo lakini ni muhimu kutafuta suluhisho kwa amani.

iii. Mtoto asipoeleweshwa mipaka yake vizuri hujisikia si salama. Mtoto anahitaji kueleweshwa mipaka yake vizuri na mlezi ili awe na msimamo, ajiamini na kujisikia salama katika lile afanyalo.

iv. Kutokuwepo kwa Wazazi au Walezi kwa muda mrefu husababisha watoto kutojisikia salama. Wazazi wengi huwa na shughuli nyingi sana ambazo huwafanya wakose muda wa kukaa na watoto.

v. Mtoto kugombezwa mara kwa mara bila maelezo yanayoeleweka humkosesha amani. Hujiona mkosefu kila siku na hujihisi kutopendwa na wazazi au walezi. Hali hii inaweza kusababisha mtoto kuamua kuondoka nyumbani, kuwa mtu asiyejipenda au kuwa mhalifu.

vi. Mzazi au Mlezi hapaswi kumuonyesha mtoto hali ya kujali vitu au kazi kuliko utu. Mtoto anahitaji sana kuwa na Mzazi au Mlezi wake. Wakati mwingine hutupa hata zawadi mbalimbali anazopewa na Mzazi/Mlezi na hujiona hapendwi na kutokuwa salama.

vii. Wazazi au Walezi ambao hawana uhakika wa usalama wao hawana uwezo wa kumhakikishia mtoto usalama. Hivyo, Mzazi au Mlezi anapaswa

kujihakikishia usalama wake kwa kupanga vizuri muda wake ili aweze kuwa na muda wa kutosha wa kulea watoto na familia.

Vilevile, yapo mambo mbalimbali ambayo hujenga hali ya usalama kwa mtoto ikiwemo:

- Upendo kati ya Baba na Mama/Walezi.
- Upendo wa Wazazi au Walezi kwa mtoto.
- Umoja na ushirikiano wa familia.
- Familia inapokuwa na utaratibu wa kufanya shughuli zao kwa pamoja.
- Watoto wanapoeleweshwa mipaka yao vizuri na kuijua.
- Wazazi au walezi kuwa na muda na nafasi ya kukaa na kuwasikiliza watoto, watoto wadogo wanahitaji pia kubebwa, mtoto mdogo hujisikia usalama zaidi pale anapobebwa na Wazazi au Walezi wake.
- Kumbeba au kumgusa mtoto unapoongea naye humjenga mtoto kisaikolojia kuweza kutosheka na kuwa na mahusiano mazuri katika jamii.
- Watoto wanahitaji kuwa sehemu ya familia inayokubalika kukiwa na hali ya kutokubalika wanakuwa na wasiwasi. Wanapopewa majukumu au nafasi na kushirikishwa katika mambo ya kifamilia hujiona kuwa wao pia ni sehemu ya familia.

**d. Kukubalika**

Watoto hujisikia hawakubaliki wakati:

i. Mzazi/Mlezi anapofoka na kulaumu kila mara.
ii. Unapomlinganisha mtoto na watoto wengine, kila binadamu ni wa pekee hivyo haipaswi kumlinganisha na mwingine.
iii. Mtoto anaposhindwa kutimiza matarajio ya wazazi au mlezi.
iv. Mlezi anapokuwa na matarajio makubwa katika mtoto kuliko uwezo wake Mzazi/Mlezi kumlaumu mtoto.
v. Mzazi/Mlezi anaposhindwa kuheshimu hisia za mtoto na utu wake au anaposhindwa kumsaidia kuelewa na kutambua tabia mbaya.

Walezi na wadau wafanye nini ili watoto walio katika mazingira hatarishi waweze kujiona wanakubalika?

- Kutambua kuwa nao ni watoto kama watoto wengine.
- Kuwawezesha kupata haki zao za msingi; chakula, mavazi, huduma za afya, malazi, elimu, usalama n.k.
- Kuwadhihirishia upendo kwa maneno, hisia na vitendo.
- Kuwakubali marafiki wao na kuwapa uhuru wa kucheza.
- Kuwasikiliza; mtoto ataelewa upendo wako kama utampa muda wa kumsikiliza.
- Kuwaheshimu.
- Kuwawezesha kukua na pia kufurahia utoto wao.
- Kutowalazimisha kuishi kama watu wazima.

**e. Kusifiwa**

Kusifiwa ni hitaji muhimu kwa kila mwanadamu. Kila mtu anaposifiwa hupenda kufanya vizuri zaidi. Mtoto ambaye hapati sifa kwa Wazazi/Walezi au jamii yake anaweza kutaka sifa kwa njia zisizo halali. Hitaji hili ni muhimu zaidi kwa watoto walio katika mazingira hatarishi ili waweze kupata matumaini, kujiamini, kujisikia wanapendwa, kutambuliwa na kukubalika. Njia nzuri/sahihi za kumsifia mtoto ni pamoja na;

i. Kumsifia mtoto kwa matendo yake mazuri, haiba yake, mafanikio yake, tabia yake nzuri na juhudi zake. Sifa kwa mtoto iwe ya kusaidia maendeleo yake. Msifie mtoto anapotimiza wajibu wake kwa mfano mtoto anapotoa zawadi/huduma kwa mtoto mwenzake ukamsifia unamjenga kitabia.
ii. Mtoto anahitaji kusifiwa na wale watu ambao ni muhimu kwake kama Wazazi au Walezi.
iii. Unapomsifia mtoto kutoka moyoni mwako yeye hujisikia vizuri.
iv. Hata yule mtoto ambaye anajaribu kufanya kitu lakini akashindwa anastahili kusifiwa kwa juhudi zake ili aendelee kujifunza.
v. Mtoto anaposifiwa hujifunza kuwa na shukurani na anaweza pia kuwasifu wengine.

**f. Kuaminiwa**

Kuaminiwa ni pamoja na:

i. Kuwapa watoto fursa ya kushiriki katika kutunza na kuhifadhi vitu mbalimbali vikiwemo vitu vyenye thamani.

ii. Kuwapa dhamana juu ya mambo mbalimbali. Watoto wanapopata fursa hiyo hujisikia kwamba wanathaminiwa na wanakubalika katika familia/jamii mfano watoto wenye mahitaji maalumu wanapokabidhiwa majukumu fulani yanayolingana na uwezo wao na kuyatimiza, hujiamini zaidi na kujiona wenye thamani katika jamii zao.

**g. Kupewa fursa ya kucheza**

Watoto walio katika mazingira hatarishi nao pia wanahitaji kucheza ili waweze kukuza na kuendeleza vipaji vyao. Michezo pia husaidia kuwapunguzia matatizo ya kisaikolojia. Michezo husisimua akili za watoto, huwafurahisha, huwachangamsha na huwafundisha mambo mengi, kwa mfano, jinsi ya kushirikiana, nidhamu, kufuata kanuni, lugha, hesabu na jinsi ya kutatua matatizo mbalimbali.

**7.5.2 Michezo ya watoto inaweza kuainishwa kwa :**

i. Kulinganisha mchango wa michezo katika ukuaji wa mtoto ; kwa mfano michezo ya kujenga tabia ya kushirikiana, michezo inayochochea fikra na ubunifu n.k.

ii. Kuangalia shughuli yenyewe inayofanywa na watoto ; kwa mfano kucheza mpira, kukimbia, kubembea, maigizo n.k. Kwa njia hizi, walezi wanaweza kutambua aina ya michezo wanayoipendelea watoto na kuwapatia fursa hiyo. Fursa ya kucheza ni pamoja na muda wa kucheza, uangalizi, nafasi ya kucheza na vifaa vya michezo, pamoja na kukuza vipaji vyake.

iii. Ni muhimu kuwaelekeza watoto ili waelewe kuwa baadhi ya michezo ni hatari kwao na jamii kwa ujumla. Watoto walio katika mazingira hatarishi wana haki sawa ya kupata fursa, vifaa, muda na nafasi ya kucheza.

iv. Michezo husaidia kujenga vipaji vyao na taratibu kupunguza au hata kuondokana na machungu, msongo na simanzi ya matukio mabaya yaliyowapata katika maisha yao.

**7.5.3 Namna ya kumsaidia Mtoto mwenye uhitaji wa Huduma ya Msaada wa Kisaikolojia na Kijamii**

i. Kubadili mtazamo wa kimazungumzo. Tambua kwamba tabia ya mtoto anayeishi katika mazingira hatarishi inachangiwa na mazingira pamoja na maisha aliyonayo/anayopitia. Kama wazazi /walezi wa watoto wanatakiwa kubadili mtazamo hasa wa jinsi ya kuongea nao kwa njia ya maswali.
ii. Tengeneza mazingira salama na rafiki kwa Mtoto.
iii. Tengeneza mahusiano imara na mtoto.
iv. Toa mifano ya mtazamo chanya wa maisha kwa mtoto.
v. Ainisha mbinu rahisi na rafiki za kumsaidia mtoto kihisia (mfano; mbinu binafsi, kupitia vikundi na kuhusisha jamii).
vi. Toa sifa kwa mtoto kwa uwezo na mabadiliko anayoonesha.
vii. Sisitiza ushirikishi wa mtoto katika kipindi chote cha kumsaidia.
viii. Ainisha na mjenge mtoto katika maeneo yake ya uwezo
ix. Mfundishe kuhusu masuala ya kimaadili na kimtazamo kulingana na jamii na mazingira yanayomzunguka mtoto
x. Kumuunganisha mtoto na huduma nyingine kwa wadau wanaotoa huduma kwa watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi. Huduma hizo zinaweza kuwa huduma za;
    - Afya kwa ujumla
    - VVU na UKIMWI
    - Kisaikolojia na kijamii
    - Madawa ya Kulevya
    - Elimu na ufundi
    - Msaada wa Kisheria n.k.

**Angalizo:**

- Kila mtoto ni wa kipekee na masuala aliyokabiliana nayo yanatofautiana na namna ya kukabiliana na kuhimili changamoto zake inatofautiana.
- Ni muhimu kuzingatia umri, hali, uelewa na ukomavu wa mtoto
- Hakikisha kuwa mtoto hadhuriki au kuongezewa maumivu kwa namna yeyote ile.
- Shirikiana na wataalamu wengine na toa rufaa kwa shauri liko juu ya uwezo wako (severe).

Ni muhimu kuzingatia mahitaji ya kihisia kwa mtoto wakati wa utoaji wa huduma za msingi kwa mtoto ili kuepuka madhara.

### 7.5.4 Athari kwa Mtoto aliyekosa Mahitaji ya Kisaikolojia na Kijamii

i. Kushindwa kujifunza

ii. Kushindwa kujenga mahusiano

iii. Kutojiamini

iv. Kutojidhatiti

v. Kutojitegemea

vi. Kuwa na hasira muda wote

vii. Kukosa uaminifu

viii. Ulemavu

ix. Kifo

x. Kujitenga

xi. Kutoroka nyumbani

xii. Kupata magonjwa mbalimbali

### 7.5.5 Athari kwa Jamii

i. Ongezeko la vitendo vya kihalifu kama ujambazi, wizi, ukabaji, uporaji na uvunjifu wa amani kwa ujumla mfano; panya road.

ii. Ongezeko la ulevi wa pombe na utumiaji wa madawa ya kulevya.

iii. Ongezeko la watoto wa wanaoishi na kufanya kazi mitaani.

iv. Ongezeko la idadi ya watoto katika ajira zenye madhara kwa watoto.

v. Ongezeko la watoto kwenye biashara ya ngono kama ukahaba, picha za ngono n.k

vi. Kuongezeka kwa maambukizi ya Virusi Vya Ukimwi, UKIMWI na magonjwa ya ngono.
vii. Kuongezeka kwa utoro na watoto wanaoacha shule.
viii. Ongezeko la vitendo vya ukatili.
ix. Ongezeko la ujinga na umaskini.

# MADA YA NANE
# HUDUMA KWA MTOTO MWENYE MSONGO

## 8.1 Muda wa kuwezesha: Dk 60

## 8.2 Malengo ya Mada

Baada ya somo hili inakusudiwa kuwa wazazi, walezi na washiriki wengine wataweza:

- Kuelewa vyanzo vya msongo
- Kueleza dalili za mtoto mwenye msongo
- Kueleza mbinu za kumsaidia mtoto mwenye msongo

## 8.3 Njia za uwezeshaji

- Bungua bongo
- Majadiliano katika vikundi
- Majadiliano ya pamoja
- Onesho mbinu/ushuhuda
- Mhadhara mfupi

## 8.4 Hatua za uwezeshaji

**Hatua ya 1:** Toa maelezo mafupi ya utangulizi juu ya mada.

**Hatua ya 2**: Waongoze washiriki kubunga bongo juu ya maana na vyanzo vya msongo.

**Hatua ya 3**: Wezesha washiriki wachache kutoa shuhuda juu ya watoto walio katika mazingira hatarishi wenye msongo na jinsi ya kuwasaidia.

**Hatua ya 4**: Vikundi viwasilishe kazi zao na yafanyike majadiliano ya pamoja/au wezesha majadiliano juu ya shuhuda zilizotolewa.

**Hatua ya 5**: Toa mhadhara mfupi juu ya dalili za msongo na jinsi ya kumsaidia mtoto aliye na msongo.

**Hatua ya 6**: Wezesha mshiriki mwenye uwezo kuhitimisha mada.

### 8.5 Maelezo ya Mada

#### 8.5.1 Kumsaidia Mtoto mwenye Msongo

#### 8.5.2 Vyanzo vya msongo

Vyanzo vya msongo ni pamoja na :

i. Migogoro ya mara kwa mara ya Wazazi/Walezi.
ii. Familia kuvunjika.
iii. Kuugua kwa wazazi kwa muda mrefu. Mtoto anaona wazazi wanavyohangaika na maumivu, anajaribu kusaidia kadri anavyoweza kulingana na umri wake. Hii humsababishia mtoto kupata msongo.
iv. Jukumu la kuuguza wazazi wao muda mrefu na mara nyingine bila msaada au rasilimali za kutosha.
v. Kunyanyapaliwa na watoto wengine, wanandugu, majirani na jamii kutokana na sababu mbalimbali.
vi. Watoto ambao wanaishi na virusi vya UKIMWI hupata shida wakati mwingine hukatazwa kwenda shule, kula na kulala na wenzao au hata kucheza.
vii. Mabadiliko ya kiuchumi yanayopelekea mtoto kukosa mahitaji muhimu au mabadiliko katika upatikanaji wa mahitaji. Ni vigumu watoto waliozoea maisha mazuri kukubaliana na mabadiliko ya ghafla, watoto wengine huacha shule kwa kukosa ada, nauli na mahitaji mengine muhimu ya shule.
viii. Kifo cha mzazi au mlezi; kifo husababisha mshtuko mkubwa sana kwa mtoto ambaye ghafla hujiona kuwa hatarini.
ix. Kuishi na virusi vya UKIMWI au magonjwa mengine ya muda mrefu pia husababisha msongo kwa watoto. Baadhi yao watakuwa wameambukizwa kupitia ubakaji, kwa hali hiyo huhitaji msaada wa ziada.

#### 8.5.3 Dalili za Mtu mwenye Msongo

i. Hasira; hukasirika haraka hata kwa vitu vidogo.
ii. Huzuni; mara nyingi hawana raha, hata kucheza hawapendi.
iii. Hofu; hupoteza imani na watu kwa kuhofia wanaweza kuwasababishia madhara mengine.

iv. Wasiwasi; hushindwa kutulia na huhangaika sana.
v. Upweke; hujitenga na watu wengine kwa kujinyanyapaa au kuhofu wengine wasimnyanyapae.
vi. Kujisikia hawafai, hawana thamani.
vii. Kusikitika kwa kutokubali hali zao, hali hii husababisha kuvunjika moyo na kukata tamaa.
viii. Kuwa na hali/dalili za kulipiza kisasi; huhisi matatizo yamesababishwa na watu. Kama jamii haijali ni rahisi kulipiza kisasi.
ix. Ushari na uchochezi wa maneno au wa vitendo. Baadhi ya watoto hugeuka wakorofi au wachochezi lakini wakisaidiwa, huweza kuondokana na hayo yote.

### 8.5.4 Jinsi ya kumsaidia Mtoto aliye katika mazingira hatarishi mwenye Msongo

Watoto wanaweza kukabiliana na msongo kama watajengewa mazingira ya kutambua uwezo walionao kama vile:

i. Uwezo wa kulielewa tukio, kwa mfano kifo au msiba.
ii. Uwezo wa kuamini kwamba wanaweza kukabiliana na tukio.
iii. Uwezo wa kulitafakari tukio na kulielewa.

### 8.5.5 Mambo ambayo yanaweza kumwezesha mtoto aliye katika mazingira hatarishi kupunguza msongo

i. Uhusiano mzuri na Mlezi/Walezi wapya na wanafamilia wengine waliobaki.
ii. Kumpatia mahitaji muhimu yakiwemo chakula, malazi, elimu, mavazi na matibabu.
iii. Kumsaidia kiuchumi.
iv. Jamii inayowazunguka kuwajali na kuwasaidia.
v. Kuwaelezea historia au kumbukumbu za kutosha juu ya watu na mambo muhimu katika familia zao na maisha yao.
vi. Kuwa na fursa za kueleza hisia zao, maono yao na kukuza vipaji vyao.

## MADA YA TISA
## MAREKEBISHO YA TABIA

**9.1 Muda wa kuwezesha:** Dk 90

**9.2 Malengo ya Mada**

Ifikapo mwisho wa mada hii washiriki wataweza:

- Kuelewa maana na lengo la marekebisho ya tabia kwa watoto
- Kuainisha tabia hatarishi na athari zake
- Kuelewa mbinu zinazotumika katika kumrekebisha mtoto tabia
- Kuelewa faida za kurekebisha tabia ya mtoto
- Mbinu za kumuadabisha mtoto

**9.3 Njia za uwezeshaji**

- Mhadhara mfupi
- Bungua bongo
- Kazi za vikundi
- Majadiliano ya pamoja

**9.4 Hatua za Uwezeshaji**

**Hatua ya 1:** Tambulisha mada.

**Hatua ya 2:** Wezesha washiriki kubungua bongo kuhusu maana na malengo ya Uchepushaji na Marekebisho ya Tabia.

**Hatua ya 3:** Wagawe washiriki kwenye vikundi na wajadili yafuatayo;

- Tabia hatarishi za Watoto na athari zake.
- Mbinu za marekebisho ya tabia.
- Faida za kurekebisha tabia ya mtoto.

**Hatua ya 4:** Wezesha washiriki kuwasilisha kazi za vikundi.

**Hatua ya 5:** Majumuisho ya mijadala.

## 9.5 Maelezo ya Mada

Marekebisho ya tabia ni mbinu ya kumwezesha mtoto kubadili tabia isiyokubalika na kuwa na tabia inayokubalika katika familia na jamii. Marekebisho ya tabia yanaanzia kwa mtoto husika, familia na jamii kwa ujumla. Kwa watoto waliokinzana na sheria au walio katika hatari ya kukinzana na sheria marekebisho ya tabia yanahusisha mamlaka mbalimbali ikiwa ni pamoja na Polisi, Mahakama, Mahabusu za Watoto, Shule ya Maadilisho na Ustawi wa Jamii.

Mpango wa Marekebisho ya Tabia ni mkakati wa Serikali ya Tanzania wa kurekebisha tabia za Watoto waliokinzana na walio katika hatari ya kukinzana na sheria, nje ya mfumo rasmi wa kisheria (Polisi, Mahakama na Mahabusu za watoto).

### 9.5.1 Malengo ya marekebisho ya tabia

- Kumsaidia mtoto kubadili tabia isiyokubalika katika jamii.
- Kubaini sababu ya mtoto kutenda kosa/makosa.
- Kumuelekeza mtoto aweze kuwa na tabia na mwenendo utakaomuwezesha kutimiza malengo na ndoto zake.
- Kuhakikisha kila inapowezekana mtoto aliyekinzana na Sheria anaishi katika mazingira ya familia wakati wa mchakato wa shauri Mahakamani au wakati anapotumikia adhabu ya Mahakama.
- Kupunguza tabia ya mtoto kurudiarudia makosa.
- Kumwezesha mtoto kuwa na maadili.

### 9.5.2 Mbinu za marekebisho ya tabia ya Mtoto

Zifuatazo ni mbinu zinazotumika katika kurekebisha tabia za watoto:

i. Kujenga mahusiano chanya kati ya Mzazi/Mlezi, familia na jamii inayomzunguka mtoto.
ii. Kubaini vipaji vya kila mtoto na kuviendeleza.
iii. Kuwashirikisha watoto kwenye shughuli mbalimbali zitakazowawezesha kujiendeleza.
iv. Kumshirikisha mtoto katika kupanga taratibu na kutekeleza shughuli mbalimbali kwa mujibu wa ratiba.

v. Kuwashirikisha watoto katika michezo mbalimbali kulingana na vipaji vyao ambayo itawasaidia kubadili tabia, mfano, vikundi vya ngoma, mpira, sarakasi, kuimba, kuigiza, kwaya, drafti na bao.
vi. Kumsifia, kumuamini, kumpongeza anapofanya vizuri, kuambatana nae katika shughuli mbalimbali.
vii. Kuongea nae, kumsikiliza na kumshauri.
viii. Kuweka mipaka ya mahusiano na majukumu.
ix. Kumueleza mtoto madhara yatakayompata kutokana na tabia alionayo.

**Angalizo:**
Shughuli zote za marekebisho ya tabia zizingatie umri, uelewa na usalama wa mtoto.

### 9.5.3 Mawasiliano chanya ya Mzazi /Mlezi na mtoto

Mzazi aimarishe mawasiliano na mtoto kwa kutumia njia mbali mbali kama vile;

i. Michezo inayoongozwa na watoto.
ii. Kumpongeza.
iii. Kumsifia.
iv. Kumshukuru.
v. Kuwapa mwitikio chanya watoto.
vi. Kumpatia zawadi.
vii. Mawasiliano ya Kihisia; aina hii ya mawasiliano inahusisha matumizi ya stadi za kusikiliza, kuongelea, kuzitaja hisia ili kusaidia watoto kuhimili na kuonyesha hisia inavyotakiwa. Mawasiliano ya kihisia husaidia watoto kujihisi wanathaminiwa, jambo ambalo husaidia kupunguza tabia isiyofaa inayosabishwa na msongo. Kwa maana hiyo Mzazi au Mlezi anapaswa kutambua na kuelewa hisia na mahitaji ya mtoto.

### 9.5.4 Mbinu za kumuadabisha mtoto

Kuna mbinu mbalimbali ambazo zinaweza kutumika kumuadabisha mtoto pindi anapokuwa amefanya makosa. Mbinu hizo ni pamoja na;

- Kumnyima fursa ya kushiriki au kufanya mambo anayoyapendelea kwa muda bila kuathiri malezi na makuzi yake, mfano kuangalia luninga, kucheza mpira, kushiriki ziara za kifamilia kama kwenda ufukweni au maonesho mbalimbali.

Aidha zipo adhabu ambazo zimekuwa zikitumika sana lakini hazishauriwi na zina madhara kwa makuzi na maendeleo ya mtoto mfano ikiwemo kumnyima mtoto haki za msingi kama chakula, kupigwa, kumfungia nje, kumfungia kwenye chumba peke yake, kuchapwa, lugha zisizofaa n.k.

### 9.5.5 Faida za Kumrekebisha Mtoto tabia

Faida za kumrekebisha mtoto tabia ni pamoja na;

i. Kumjengea tabia ya kujiamini na kufanya mambo mengi bila ya kushurutishwa.
ii. Inamuwezesha kushiriki katika shughuli za kifamilia na kijamii.
iii. Inamwezesha mtoto kutoa maamuzi sahihi.
iv. Kumsaidia na kumuwezesha mtoto kuwa na tabia na mwenendo unaokubalika katika jamii.
v. Kumsaidia mtoto kujifunza kujiepusha na tabia hatarishi zisizokubalika katika jamii.
vi. Inamwandaa mtoto kuweza kujisimamia na kuwa kiongozi bora wa baadae.
vii. Inamuepusha na tabia zinazoweza kusababisha aingie kwenya mkinzano na sheria.
viii. Inapunguza uwezekano wa watoto kujiingiza katika mazingira hatarishi.
ix. Inatoa fursa kwa mtoto kushiriki katika shughuli za kijamii na kuendelea na masomo.
x. Kumsaidia mtoto kutorudia rudia kutenda makosa.

## MADA YA KUMI
## UTAMBUZI WA WADAU

**10.1 Muda wa kuwezesha:** Dk 90

### 10.2 Malengo ya Mada

Ifikapo mwisho wa mada hii washiriki wataweza:

- Kutambua wadau walioko katika maeneo yao
- Kubaini huduma zinazotolewa na wadau mbalimbali walioainishwa , pamoja na maeneo wanayohudumia
- Kufahamu umuhimu wa wadau katika kusaidia utoaji wa huduma

### 10.3 Njia za uwezeshaji

- Mihadhara mifupi
- Bungua bongo
- Majadiliano katika vikundi vidogo
- Majadiliano ya pamoja

### 10.4 Vifaa vya kuwezeshea

- Bango kitita
- Kalamu za wino mzito
- Vitini vya sheria
- Projecta

### 10.5 Hatua za kuwezesha

**Hatua ya 1:** Toa mhadhara mfupi kuhusu malengo ya mada.

**Hatua ya 2:** Wagawe washiriki katika vikundi kulingana na sehemu wanazotoka na wafanye yafuatayo:

- Waorodheshe wadau walioko ndani na nje ya maeneo yao.
- Waainishe huduma zinazotolewa na kila mdau.
- Wachore mchoro wa chapati kuonesha nafasi na umuhimu wa mdau. Umuhimu wa mdau utaoneshwa kulingana na ukubwa wa chapati na nafasi itaonesha ukaribu wa mdau na Mlezi wa kuaminika.

**Hatua ya 3**: Wezesha vikundi kuwasilisha kazi zao.

**Hatua ya 4:** Hitimisha kwa kuelezea umuhimu wa wadau katika kusaidia utoaji wa huduma.

## 10.6 Maelezo ya Mada

Katika kusaidia utoaji wa huduma Mlezi wa kuaminika kwa kushirikiana na Afisa Ustawi wa Jamii wanapaswa kutambua wadau mbalimbali ambao wanaweza kusaidia katika utoaji wa huduma katika maeneo yao. Miongoni mwa wadau hao ni kama wanavyoonekana katika mchoro hapo chini (Angalia mchoro na.1) .

### 10.6.1 Baadhi ya wadau wanaoweza kusaidia utoaji wa huduma kwa watoto

i. Ofisi ya Ustawi wa Jamii
ii. Ofisi ya Maendeleo ya Jamii
iii. Ofisi ya Mtendaji wa Kata
iv. Ofisi ya Mtendaji wa Kijiji /Mtaa
v. Ofisi ya elimu
vi. Zahanati
vii. Afisa Lishe
viii. Kituo cha Polisi
ix. Kituo cha Afya
x. Mahakama
xi. Asasi za kiraia
xii. Misikiti
xiii. Kanisa
xiv. Vikoba
xv. Mhabusu ya Watoto
xvi. Vituo vya kulelea watoto wadodo mchana
xvii. Makao ya watoto
xviii. Mlezi wa kuaminika
xix. Shule ya Maadilisho
xx. Nyumba salama

xxi. Nyumba za waraibu
xxii. Magereza
xxiii. Uhamiaji
xxiv. Kamati za MTAKUWWA
xxv. Wasaidizi wa kisheria

### 10.6.2 Umuhimu wa Wadau

Wadau ni muhimu katika kusaidia upatikanaji wa huduma mbalimbali zikiwemo;

i. Msaada wa kisheria
ii. Malezi ya kiroho
iii. Huduma za Elimu
iv. Huduma za Afya
v. Huduma za lishe
vi. Huduma za utengamao
vii. Rufaa
viii. Marekebisho ya tabia
ix. Msaada wa afya ya akili, kisaikolojia na kijamii
x. Kuimarisha uchumi wa kaya
xi. Huduma za unasihi na ushauri

### 10.6.3 Majukumu ya wadau

i. Kutoa elimu.
ii. Kutoa ushauri wa kitaalam.
iii. Kufanya ufuatiliaji na tathmini.
iv. Kutoa huduma muhimu kama matibabu, mavazi,vifaa vya elimu, malazi, makazi, chakula, vifaa visaidizi kwa watoto wenye ulemavu au mahitaji maalum.
v. Kuwaunganisha watoto na familia zao,ndugu ,jamaa, kutoa msaada wa Afya ya Akili, Kisaikolojia na Kijamii.
vi. Kuwasaidia familia kiuchumi kuwapatia mikopo na kuwaunganisha na fursa zilizopo katika jamii.

vii. Kusimamia haki za watoto kwenye vyombo vya sheria.

**Jedwali Na. 3: Mfano wa jedwali la kutambua wadau na huduma zao**

| Na. | Eneo | Mdau | Huduma |
|---|---|---|---|
| 1. | | | |
| 2.. | | | |
| | | | |
| | | | |

**Mchoro Na. 1: Mchoro wa vein**





Figure 10:1 1

## MADA YA KUMI NA MOJA
## KUIMARISHA UCHUMI WA KAYA

**11.1 Muda wa kuwezesha:** Dk 120

### 11.2 Malengo ya Mada

Ifikapo mwisho wa mada hii washiriki wataweza:

- Kutambua na kutumia rasilimali zilizopo katika mazingira yao wa ajili ya kujiongezea kipato
- Kuelewa mambo muhimu katika kubuni, kuanziasha, kuendesha na kusimamia miradi midogomidogo itakayosaidia kuongeza kipato
- Kuelewa umuhimu wa kujiunga katika vikundi vya ujasiliamari Kuwatambua wataalam waliopo katika ngazi ya jamii wanaoweza kuwasaidia kubuni kuanzaisha na kuendesha miradi pia kuwaunganisha na wadau/taasisi/ vikundi vinavyotoa mikopo isiyo na masharti magumu
- Kutambua wadau na wajibu wao katika shughuli za vikundi za kuinua kipato cha kaya

### 11.3 Njia za uwezeshaji

- Mhadhara mfupi
- Bungua bongo
- Kazi za vikundi
- Majadiliano ya pamoja

### 11.4 Hatua za kuwezesha

**Hatua ya 1:** Toa maelezo mafupi ya utangulizi wa mada.

**Hatua ya 2**: Ongoza washiriki kubungua bongo kuhusu maana ya rasilimali.

**Hatua ya 3**: Wagawe washiriki katika vikundi kubaini aina za rasiriamali zilizopo katika maeneo yao na aina ya miradi wanayoweza kutekeleza kwa kutumia rasilimali hizo ili kujiongezea kipato.

**Hatua ya 4**: Ongoza washiriki kuwasilisha kazi za vikundi na kufanya mjadala wa pamoja.

Hatua ya 5; Wagawe washiriki katika vikundi kujadili na kubaini Taasisi /Vikundi

**Hatua ya 6:** Waongoze washiriki kubungua bongo kuhusu vyanzo vya mitaji.

**Hatua ya 6**: Toa ufafanuzi kuhusu mambo muhimu ya kuzingatia katika uendeshaji wa miradi ya kiuchumi, wape washiriki nafasi ya kutoa uzoefu kuhusu shughuli mbalimbali wanazozifanya za kujiongezea kipato.

**Hatua ya 7:** Ongoza majadiliano kuhusu umuhimu wa kujiunga na vikundi vya ujasiriamali.

**Hataua ya 8**: Wagawe washiriki kwenye vikundi na wawezeshe kuchagua mradi mmoja wa mfano na kuufanyia uchambuzi na kisha kuandaa mpango wa utekelezaji

**Hatua ya 9:** Waongoze washiriki kuwasilisha kazi za vikundi.

## 11.5 Maelezo ya Mada

### 11.5.1 Maana ya rasilimali

Rasilimali ni nyenzo za msingi zilizopo katika mazingira wanamoishi jamii ikiwa ni pamoja na ardhi, maji, madini, mifugo, watu na wataalam. Rasilimali hizo zinaweza kutumika kama mtaji wa kuanzisha na kuendeleza mradi wa kiuchumi.

### 11.5.2 Aina za rasilimali

**Ardhi**: Inatumika kwa ajili ya kilimo, ujenzi wa nyumba, kufugia, kujenga barabara n.k

**Maji**: Yanatumika kwa ajili ya matumizi ya binadamu, umwagiliaji kwenye kilimo, Ufugaji wa samaki n.k

**Watu**: Hawa ndiyo nguvu kazi katika uzalishaji na pia wanatoa utaalam kwa ajili ya shughuli za ugani.

**Fedha**: Fedha zinatumika kama mtaji kwa ajili ya uanzishwaji wa mradi.

### 11.5.3 Namna ya kubuni na kuendesha miradi midogomidogo itakayosaidia kuongeza kipato katika Kaya

Familia zinahitaji kujengewa uwezo namna ya kujipatia kipato kwa ajili ya kujiendeshea maisha yao ya kila siku, hivyo mbinu sahihi za uibuaji na uendeshaji miradi midogomidogo kwa kutumia rasilimali zinazowazunguka zinahitajika.

Mbinu hizo ni pamoja na utambuzi wa rasilimali zilizopo katika eneo wanaloishi, mafunzo ya ujuzi wa yakiwemo mapato, matumizi ya fedha na akiba pamoja na kupanga mipango na bajeti ya familia.

### 11.5.4 Masuala ya kuzingatia wakati wa kuanzisha mradi

i. Kuwepo kwa wazo la mradi; ni mradi wa aina gani unafaa kulingana na uwezo wa mwanzishaji na mazingira ya sehemu husika.
ii. Kufanya upembuzi yakinifu ili kuangalia uwepo wa soko la bidhaa, gharama za uzalishaji, faida unayotegemea kuipata na mtaji iwapo utatosha kutekeleza mradi.
iii. Andaa Mpango wa Kutekeleza mradi. Mpango uainishe aina ya mradi, gharama za uendeshaji, mbinu za utekelezaji, faida tarajiwa na tahadhari za mradi. Ni muhimu mpango wa utekelezaji kuonyesha malengo unayotaka kufikia katika vipindi mbalimbali vya utekelezaji wa mradi.
iv. Hakikisha mkopo unaoupata kwa ajili ya biashara unatumika kwa ajili ya biashara husika na unafanya marejesho kwa wakati.
v. Hakikisha unaweka vizuri kumbukumbu za mapato na matumizi (mali bila daftari hupotea bila habari).
vi. Hakikisha anatunza mtaji na kuweka akiba.

**Angalizo:**
Si vema kuiga miradi inayofanywa kwa mafanikio na watu wengine bila kufanya utafiti. Pia kuzingatia uwezo wa kifedha ulio nao.

### 11.5.5 Umuhimu wa kujiunga katika vikundi vya kiuchumi na biashara ndogo ndogo kwa lengo la kuimarisha uchumi wa Kaya /Familia

i. Ni rahisi kupata mikopo kwa ajili ya mitaji ya biashara.
ii. Ni rahisi kupata utaalam katika kubuni, kuanzisha na kuendesha miradi.
iii. Inasaidia kupata masoko ya bidhaa zitakazozalishwa.
iv. Kujenga mahusiano ya kibiashara na uaminifu na taasisi za kifedha.
v. Kuimarisha mahusiano na kujifunza mipango na shughuli mbalimbali za kiuchumi katika jamii.
vi. Kuimarisha upatikanaji wa huduma mbalimbali katika familia.

**Jedwali Na. 4: Wajibu wa wadau katika kuwezesha shughuli za vikundi vya kiuchumi katika jamii**

| Na. | Wadau | Wajibu |
|---|---|---|
| 1. | Taasisi za kifedha (Benki, vikundi vya kuweka na kukopa - VICOBA) | Kutoa mikopo, kuweka akiba, elimu ya biashara na ushauri. |
| 2. | Vikundi vya kijamii | • Ushauri, elimu ya biashara na masoko.<br>• Kuweka akiba na kutoa mikopo. |
| 3. | Idara ya Maendeleo ya Jamii | • Kutoa Mikopo, elimu ya ujasiriamali katika vikundi.<br>• Kutoa Ushauri<br>• Usajili wa vikundi na kufunga vikundi vinavyokiuka masharti ya mikopo.<br>• Kufanya ufutiliaji wa marejesho.<br>• Kuhifadhi kumbukumbu za mikopo. |
| 4. | Kitengo cha biashara (Halmashauri) | • Kutoa leseni za biashara.<br>• Kutoa ushauri kuhusu kodi. |
| 5. | Asasi za kiraia na kidini | • Kutoa elimu ya biashara na ushauri.<br>• Mikopo na masoko |
| 6. | SIDO na VETA | Kutoa elimu ya biashara na ushauri. |
| 7. | Sekta binafsi | Kutoa mikopo, ushauri na masoko. |

## MADA YA KUMI NA MBILI
## HUDUMA KWA WATU WENYE ULEMAVU

**12.1 Muda wa kuwezesha:** Dk 120

**12.2 Malengo ya Mada**

Ifikapo mwisho wa mada hii washiriki wataweza kuelewa:

- Mtoto mwenye ulemavu
- Haki za mtoto mwenye ulemavu
- Utambuzi wa awali wa mtoto mwenye ulemavu
- Vyanzo na aina za ulemevu
- Namna ya kuzuia ulemavu
- Mahitaji ya mtoto mwenye ulemavu
- Jinsi ya kumsaidia mtoto mwenye ulemavu

**12.3 Njia za uwezeshaji**

- Bungua bongo
- Majadiliano katika vikundi
- Majadiliano ya pamoja
- Muhadhara mfupi

**12.4 Hatua za kuwezesha**

**Hatua ya 1**. Toa maelezo ya utangulizi wa mada.

**Hatua ya 2**. Waongeze washiriki kujadili kwenye vikundi kuhusu:

- Maana ya mtoto mwenye ulemevu
- Vyanzo vya ulemevu
- Aina za ulemavu
- Jinsi na sababu za utambuzi wa awali wa mtoto mwenye ulemavu
- Namna ya kuzuia ulemavu
- Haki za mtoto mwenye ulemavu
- Mahitaji ya mtoto mwenye ulemavu
- Jinsi ya kumsaidia mtoto mwenye ulemavu

**Hatua ya 3**. Waongoze Washiriki kuwasilisha kazi za vikundi.

**Hatua ya 4**. Ongoza majadiliano ya pamoja kutokana na masuala yatakayoibuliwa kwenye uwasilishaji wa kazi za vikundi.

**Hatua ya 5**. Hitimisha kwa kutoa maelezo na ufafanuzi kulingana na hoja zilizojadiliwa.

## 12.5 Maelezo ya Mada

### 12.5.1 Mtoto mwenye ulemavu

Ni mtoto ambaye ana tatizo la kimwili, kiakili au kihisia ambalo linazuia au kupunguza ushiriki wake katika mambo ya kijamii akilinganishwa na Watoto wengine wasio na ulemevu hasa anapokabiriana na vikwazo kwa mujibu wa Sera ya Taifa ya Maendeleo na Huduma kwa Watu wenye Ulemevu ya mwaka 2004.

### 12.5.2 Haki za watoto wenye ulemavu

Haki ni stahili ambazo Mtoto anapaswa kupatiwa. Haki za Watoto zimegawanyika katika makundi makuu manne ambayo ni:

i. Haki ya kulindwa (kuwa na wazazi/ walezi, kupata matunzo, kutobaguliwa, kutonyanyaswa, kupata hifadhi, kutambuliwa utaifa).
ii. Haki ya kuishi (kupata huduma za afya, chanjo, lishe, malazi, kutambuliwa).
iii. Haki ya kushiriki na kushirikishwa (kusikilizwa, kutoa maoni).
iv. Haki ya kuendelezwa (kupata elimu, kucheza, kupata habari, malezi/ maadili, kufahamu mila na desturi).

### 12.5.3 Utambuzi wa awali wa mtoto mwenye ulemavu

i. Rangi ya ngozi ya Mtoto.
ii. Kichwa cha mtoto kama kina ukubwa wa kawaida.
iii. Shingo ya Mtoto kama inazunguka inavyotakiwa.
iv. Macho ya Mtoto kama mboni ni nyeupe au iko kama mawingu.
v. Uwazi kwenye mdomo wa juu.
vi. Mikono na miguu ya Mtoto kutokunjika au kunyooka sawasawa.
vii. Mikono na miguu kutokuwa na nguvu.

viii. Mtoto baada ya kuzaliwa kuwa na alama, vidonda au uvimbe mgongoni na mabaka kichwani.

ix. Sehemu ya haja ndogo na kubwa ya Mtoto haziko sawa.

### 12.5.4 Vyanzo vya ulemavu

i. Magonjwa (Mfano Athari za Ukoma, Polio, Surua na Magonjwa ya ngono).

i. Changamoto wakati wa kujifungua.

ii. Ajali (wakati na baada ya kuzaliwa). Ajali wakati wa kujifungua ni kama vile mtoto kudondoka, kuvutwa kupitiliza ambayo huadhiri mishipa ya fahamu.

iii. Uchungu pingamizi /kuchelewa kujifungua ambao husababisha ukosefu wa oksini kwa mtoto na kuadhiri ubongo ambao huongoza utendaji kazi wa mishipa ya fahamu na misuri.

iv. Matibabu yasiyo sahihi ambayo huathiri mishipa ya fahamu mfano uchomaji mbaya wa sindano.

v. Mama Mjamzito kutumia vileo, mionzi na madawa bila ushauri wa Wataalamu

vi. Urithi (Mfano Ualbino).

vii. Msongo wa mawazo.

viii. Kasoro katika chembe hai (Mfano Ulemavu wa Viumbe, Akili na Usonji)

ix. Lishe duni kwa mama mjazito na mtoto.

x. Mtoto na Mama Mjazito kukosa chanjo muhimu.

xi. Mama Mjamzito kutojifungulia katika Vituo vya Kutolea Huduma za Afya.

### 12.5.5 Aina za Ulemavu

i. Kiziwi,

ii. kutokuona na uoni hafifu

iii. Ulemavu wa akili

iv. Mtindio wa ubongo.

v. Ulemavu wa viungo (mikono, miguu, kupinda kwa mifupa, uti wa mgongo).

vi. Ulemavu mchanganyiko.

vii. Usonji.

viii. Ualbino.

ix. Kichwa kikubwa na mgogo wazi.

x. Down syndrome (mfano maumbile yao yanafanana kama vile sura, kichwa cha mviringo)

### 12.5.6 Namna ya kuzuia Ulemavu

i. Zingatia umri wa kubeba mimba (mama asiwe na umri wa chini ya miaka 18 na zaidi ya 35).

ii. Anza kupata huduma za afya ya uzazi mapema ikiwezakana kabla ya ujauzito.

iii. Zingatia chakula bora kipindi chote cha ujauzito.

iv. Kuhudhuria kliniki kipindi chote cha ujauzito.

v. Kutotumia bidhaa za tumbaku, dawa za kulevya, pombe na dawa za asili.

vi. Kuepuka matumizi ya mionzi bila ushauri wa daktari.

vii. Kuhakikisha mama mjamzito anajifungua katika kituo cha kutolea huduma za afya.

viii. Kumnyonyesha mtoto ndani ya saa moja baada ya kujifungua.

ix. Mtoto anyonyeshwe maziwa ya mama pekee kwa muda wa miezi 6.

x. Mtoto apatiwe lishe sambamba na maziwa ya mama baada ya miezi 6.

xi. Mtoto apelekwe kliniki ili apatiwe chanjo zote muhimu.

### 12.5.7 Vifaa vya kujimudu /visaidizi

Hivi ni vifaa ambavyo husaidia kurahisisha maisha ya Mtoto mwenye Ulemavu wa viungo na kumuwezesha kumudu mazingira. Vifaa hivi ni kama vile kiti mwendo, baiskeli ya miguu mitatu, magongo, miguu ya bandia, viatu maalum na viungo bandia kama vile mkono na mguu bandia.

**Mchoro Na. 2: Vifaa vya kujimudu/visaidizi**

| | | |
|---|---|---|
|  |  |  |

#### 12.5.8 Tiba

Tiba za urekebishaji wa kitaalam kwa Mtoto mwenye Ulemavu wa viungo hufanyika kama vile upasuaji.

#### 12.5.9 Lishe

**Kwa mama mjamzito**

i. Ale mlo kamili wenye mchanganyiko wa makundi yote matano ya chakula ambayo ni nafaka, asili ya kunde na nyama, mbogamboga, matunda na mafuta.
ii. Ale milo mitatu kwa siku na kuwa na milo ya ziada.
iii. Aanze kliniki mapema mara tu anapogundua ni mjamzito.
iv. Apewe vidonge vya madini ya chuma na foliki asidi kipindi chote cha ujauzito hadi miezi mitatu baada ya kujifungua.
v. Apate muda wa kupumzika.
vi. Atumie chumvi yenye madini joto.

**Kwa mtoto**

i. Aanze kunyonyeshwa maziwa ya mama mara tu anapozaliwa ndani ya saa moja ya kwanza na aendelee kunyonyeshwa maziwa ya mama pekee kwa kipindi cha miezi sita ya mwanzo. Baada ya miezi sita Mtoto aendelee kunyonya hadi miaka miwili na apewe chakula cha nyongeza.
ii. Chakula cha nyongeza kiwe mlo kamili toka makundi yote matano ya chakula.
iii. Mtoto apate jua la asubuhi ili kuuwezesha mwili wake kutengeneza vitamini D.
iv. Apelekwe kliniki na kupata chanjo kama inavyoelekezwa.

### 12.6 Unasihi

Unasihi humwezesha Mtoto mwenye Ulemavu mwenyewe, wazazi na jamii kukubali na kukabili hali ya ulemavu. Pia kutoa elimu kuhusu mila potofu zinazoweza kukwamisha utoaji wa afua stahiki.

**i. Elimu**

Unasihi humwezesha Mtoto mwenye Ulemavu mwenyewe, wazazi na jamii kukubali na kukabili hali ya ulemavu. Pia kutoa elimu kuhusu mila potofu zinazoweza kukwamisha utoaji wa afua stahiki.

**ii. Utetezi na uzengezi**

Utetezi na uzengezi ni muhimu kwa Mtoto mwenye Ulemavu wa viungo ili kuweza kushauri na kushawishi wadau mbalimbali juu ya Sera, Sheria Miongozo, huduma na haki stahili.

**iii. Mazingira rafiki**

Ni muhimu kutengeneza mazingira rafiki yatakayowezesha ujongeaji kwa Mtoto mwenye Ulemavu ili aweze kufikia huduma au mahitaji muhimu. Mazingira hayo ni kama uwepo wa majengo yenye lifti, vyoo vya kukaa, na ngazi mtelezo (angalia mchoro unaofuata).

**Mchoro Na. 3: Mfano wa mazingra rafiki kwa mtoto mwenye ulemavu**



**iv. Huduma za afya**

Watoto wenye Ulemavu wana haki sawa kama watoto wengine kupata huduma bora za afya, ikiwa ni pamoja na huduma stahiki za VVU na UKIMWI ambazo ni pamoja na kupima VVU na iwapo wana maambukizi kuunganishwa na huduma za tiba na matunzo.

**12.6.1 Uchangamshi wa awali kulingana na aina ya ulemavu**

Ni vitendo vya makusudi vinavyolenga kumpa Mtoto fursa ya kushiriki kikamilifu katika kutenda ,kuwa na mahusiano bora nawtu,matukiona vitu mbalimbali katika mazingira anamoishi kama msingi muhimu wa ukuaji na jifunzaji.

i. Kuwapa mahitaji muhimu kwa Watoto wenye Ulemavu kama chakula, mavazi na malazi

ii. Kuzingatia usafi wa mwili na mazingira anayoishi Mtoto mwenye Ulemavu.
iii. Kumpeleka mapema Mtoto mwenye Ulemavu katika vituo vya kutolea huduma za afya na marekebisho.
iv. Kuwa na mazingira rafiki kwa Mtoto mwenye mahitaji maalum (mfano vyoo maalum, ngazi mtelezo).
v. Kuwakinga/kutokuwafanyia vitendo vya ukatili wa kijinsia/ukatili dhidi ya watoto.
vi. Kuwatambua wadau mbalimbali wanaotoa huduma kwa Watoto wenye Ulemavu.
vii. Kutambua maeneo ya utolewaji wa huduma mbalimbali na kutoa rufaa kulingana na mahitaji ya Mtoto.